Haliuzwi
FEBRUARI 17, 2026
/islamicftz
Ramadhan 7 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 572
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Samia aahidi jeshi imara na la kisasa, azindua Makao Makuu ya Ulinzi ya Sh318.8 bilioni

Msimu mashindano ya Qur'an wazinduliwa kwa kishindo

Mkurugenzi wa taasisi ya The Islamic Foundation, Mkoa wa Mwanza, Abdulhakim Abeid akikabidhi zawadi kwa mmoja wa washindi wa mashindano ya Qur'an kwa madrasa 41 za mkoa wa Mwanza yaliyofanyika katika Msikiti wa Abeid.

- Sheikh Kombo Ali Fundi: Wanaojihusisha na Qur'an, hususan wenye kuihifadhi, waipe haki yake kwa kuonesha tabia nzuri
- Sheikh Muhammadayn: Shikamana na Qur'an Allah akupandishe daraja

يا أيها الذين آمنوا كتب عليكم الصيام كما كتب على الذين من قبلكم

Rais Dkt. Mwinyi: Malezi ya vijana yaanzie kwenye mafundisho ya Qur'an

Zanzibar yadhamiria kupunguza utegemezi kwa wafadhili

Tuhoji uhalali wa nembo "Halal" au tuamini tu?

Dubai vipimo vya afya bure mwezi mzima wa Ramadhan

Je, ni lazima kunuizwa kufunga Ramadhan?

UKHTI FATIMA SS

Shikamana na Qur'an Allah akupandishe daraja -Sheikh Muhammadayn

Waislamu wamehimizwa kushikamana na Qur'an kwani yoyote anayeshikamana na kitabu hicho Mwenyezi Mungu humpa utukufu, humpandisha daraja na kumheshimisha.

Kauli hiyo imetolewa na Sheikh Hassan Muhammadayn alipokuwa akizungumza na Waislamu waliojitokeza katika mashindano ya Qur'an kwa madrasa za mkoa wa Mwanza yaliyofanyika katika Msikiti wa Abeid.

Sheikh huyo, aliyealikwa kama mgeni rasmi, alionya pia kuwa mtu akiipuuza Qur'an, basi Allah Aliyetukuka atamdhalilisha na kumtupilia mbali.

Akinukuu hadith ya Mtume, Sheikh Muhammadayn alisema Mwenyezi Mungu, kupitia Qur'an, anawainua watu daraja za juu duniani na akhera, lakini pia kuna watu watadhalilishwa na kudunishwa kwa sababu wameipuuza, wameihama na hawajaifanyia kazi Qur'an.

Sheikh Muhammadayn alisema Qur'an ni miongoni mwa mambo ambayo yanapaswa kuwashughulisha sana Waislamu katika Ramadhan kwa sababu imeshushwa katika mwezi huo. Alitaja namna za kujishughulisha na Qur'an kuwa ni pamoja na kuisoma kwa wingi, kuizingatia sana, kuifanyia kazi kama inavyotakiwa na kusikiliza kwani hata Mtume alipenda kusikiliza Qur'an.

Sheikh alinukuu hadith zinaonesha kuwa Mtume aliomba asomewe Qur'an ili asikilize lakini pia alipomsikia Abu Musa al-Ash'ary akisoma Quran ndani ya nyumba yake akamsifu kuwa amepewa sauti nzuri ya kusoma Qur'an kama aliyopewa Nabii Daud aliyekuwa akisomea Zaburi.

"Kwa hiyo Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa mpenzi wa kusikiliza Qur'an na pale anapomsikia mtu anasoma Qur'an na ana sauti nzuri, pia alikuwa anampa maua yake, anamsifia," alisema Sheikh Muhammadayn.

Akizungumza kuhusu mashindano hayo, Sheikh alisifu juhudi zilizofanyika akitanabaisha kuwa licha ya uchanga wa vijana ambao baadhi na woga, mashindano hayo yalikuwa ni mwanzo mzuri.

"Ukiangalia wote hawa waliokuja, naamini, ni madrasa za mtaani kwa maana, ni wale wanafunzi ambao muda mrefu wanakuwa mashuleni na muda mdogo wanaoupata ndio wanakuja madrasa. Kwa hiyo juhudi zilizofanyika ni kubwa na za muda mdogo hivyo tunapaswa kuwasifu wasimamizi wa madrasa, walimu na wanafunzi"

Katika mashindano hayo, madrasa 41 ziliingia katika mashindano ni 17 ndio ziliingia katika mchakato rasmi, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa taasisi ya The Islamic Foundation, Mkoa wa Mwanza, Abdulhakim Abeid.

Akizungumza katika hafla hiyo, Abeid alisema wanatarajia kuboresha zaidi mashindano hayo mwakani, ikiwemo kuongeza juzuu za kushindaniwa hadi walau 15 kutoka za sasa tano na pia kuweka nguvu kubwa kwa wanawake pia.

Naye Sheikh Kombo Ali Fundi, akizungumza katika hafla hiyo aliwataka wanaojihusisha na Qur'an, hususan wenye kuihifadhi, waipe haki yake kwa kuonesha tabia nzuri.

"Wote tunatakiwa tuwe watu wazuri lakini waliohifadhi Qur'an ni watu wa aina yake. Inatakiwa mtu akiambiwa huyu amehifadhi Quran, anasema ni kweli na mimi nataka nimuige," alisema Sheikh Kombo.

رمضان

MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpiga Picha Wetu

Mashindano ya Qur'an kwa madrasa 41 za mkoa wa Mwanza yaliyofanyika katika Msikiti wa Abeid

رمضان

MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpiga Picha Wetu

Mashindano ya Qur'an kwa madrasa 41 za mkoa wa Mwanza yaliyofanyika katika Msikiti wa Abeid

NA YUSUPH AMIN

Msimu mashindano ya Qur'an wazinduliwa kwa kishindo

Mwishoni mwa juma hili, Waislamu nchini Tanzania wametumia muda wao mwingi kufuatilia fungua dimba ya mashindano ya Qur'an katika ngazi mbalimbali.

Mashindano hayo katika siku za mwisho wa wiki za juma la kwanza la Ramadhan ya mwaka huu yanaashiria kufunguliwa pazia la mashindano hayo ambayo hutawala mwezi mzima wa Ramadhan.

Moja kati ya mashindano yaliyofuatiliwa sana Jumapili ya Februari 22, 2026 ni lile la ngazi ya kitaifa, lililoandaliwa na taasisi ya Aisha Sururu Foundation (ASF) ambapo mgeni rasmi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti na Baraza la Mapinduzi, Dkt Hussein Ali Mwinyi aliwahimiza Waumini wa dini ya Kiislamu kuongeza juhudi katika ibada ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan na kuendeleza matendo ya huruma na ukarimu kwa kuwasaidia wenye uhitaji, wajane na yatima ili kuimarisha mapenzi na amani katika jamii.

Dkt. Mwinyi alisema kuwa mashindano hayo yanadhihirisha mshikamano wa kitaifa, akieleza kuwa ni jukwaa muhimu la kukuza vipaji vya usomaji wa Qur'an nchini na kuimarisha msingi wa kiimani kwa vijana.

Katika hotuba yake, Dkt. Mwinyi alipongeza taasisi ya Aisha Sururu Foundation pamoja na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata) kwa ushirikiano wao, na kuwapongeza walimu, masheikh na majaji kwa juhudi zao na uadilifu katika kuwaandaa washiriki.

Awali akitoa taarifa ya mashindano hayo, mwakilishi wa Bi Aisha Sururu Foundation alisema taasisi hiyo itaendelea kuandaa mashindano kila mwaka ili kuwapa vijana nafasi ya kuonesha vipaji vyao na kujijengea misingi imara ya dini.

Aliongeza kuwa Qur'an ni mwongozo wa maisha hivyo vijana wanapojifunza na kuihifadhi wanajenga jamii yenye amani, mshikamano na heshima.

Zawadi kwa washindi

Washiriki wa kike na kiume kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani walishiriki katika ngazi tofauti za mashindano hayo kuanzia juzuu 3, 5, 10, 20 hadi 30. Katika hatua ya fainali ushindani ulikuwa mkali huku washiriki wengi wanaotokea jijini Dar es Salaam wakiibuka washindi baada ya kuonesha uwezo wa hali ya juu katika kusoma na kuhifadhi Qur'an,

Kwa upande wa wavulana, kijana Said Rashid Bakari kutoka Dar es Salaam aliibuka mshindi wa kwanza kwa waliohifadhi juzuu 30 na kuchukua kitita cha shilingi milioni 5 za Kitanzania baada ya kupata alama 97.75. Nafasi ya pili ilishikwa na Hilary Khamisi Hamadi kutoka Pemba aliyepata shilingi milioni 4 na nusu, na wa tatu ni Amri Bakari Abdallah aliyejinyakulia jumla ya shilingi milioni 4.

Kwa upande wa wasichana, mshindi wa kwanza wa juzuu 30 ni Fat–hia Ally Abdallah aliyezawadiwa shilingi milioni 5, wa pili ni Time Mohammed Mwinyi aliyepata milioni 4 na nusu, na wa tatu ni Asmaa Rubea Saleh aliyepata milioni 4.

Walioibuka washindi wa kwanza kwa upande wa washiriki wa juzuu 3 hadi 20 wanaume ni Swabi Mwalimu Abbas (juzuu 20) aliyezawadia milioni 4, Zaidu Alawi Hamadi (juzuu 10) milioni tatu, Faaris Alawi Hamadi (juzuu 5) aliyepata milioni 2, na Akram Abdallah Khamisi (juzuu 3) akishinda milioni moja.

Kwa upande wa wasichana, mshindi wa kwanza juzuu 20 ni Kauthar Al–Amin Swaleh aliyepewa milioni 4, juzuu 10 Nasra Nassor Suleiman aliyejinyakulia milioni 3, juzuu 5 Yusra Jumaa Saleh aliyepata milioni 2, na juzuu 3 ni Najma Ahmadi Shaha aliyepata milioni moja. Mbali na zawadi kwa washindi, mashindano hayo pia yaliambatana na utoaji wa Tuzo Maalum ya heshima kwa Marhum Mzee Ali Hassan Mwinyi, ambapo Rais Dkt. Mwinyi alipokea tuzo hiyo kwa niaba yake.

Shindano hilo ni miongoni mwa mashindano makubwa ya Qur'an yanayofanyika kila mwaka ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan na kuvutia watu wengi kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Mashindano hayo ambayo mwaka huu yamefanyika kwa mara ya 26 yalihusisha pia washiriki kutoka makundi maalum wakiwamo wenye ulemavu huku walimu wa washindi wa juzuu 30 wakipewa zawadi ya tiketi za kwenda Umrah, ikiwa ni ishara ya kutambua kazi wanayoifanya katika kuendeleza Qur'an.

Akizungumza katika mashindano hayo yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam, Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi alisisitiza umuhimu wa kuendeleza utamaduni wa kuisoma, kuihifadhi na kuzingatia mafundisho ya Qur'an Tukufu ili kujenga kizazi chenye maadili, hofu ya Mwenyezi Mungu na mchango chanya kwa jamii.

NA MWANDISHI WETU

Mwinyi: Malezi ya vijana yaanzie kwenye mafundisho ya Qur'an

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesisitiza umuhimu wa vijana kuisoma, kuihifadhi na kuzingatia mafundisho ya Qurani Tukufu ili kujenga kizazi chenye maadili, hofu ya Mwenyezi Mungu na mchango chanya kwa jamii.

Rais Dkt. Mwinyi ameyasema hayo katika Mashindano ya Kitaifa ya Qurani Tukufu yaliyoandaliwa na Taasisi ya Aisha Sururu Foundation, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam na kuwakutanisha washiriki kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Aidha, Rais Dkt. Mwinyi ameipongeza taasisi hiyo pamoja na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kwa kuendeleza mashindano hayo, akieleza kuwa ni jukwaa muhimu la kukuza vipaji na kuimarisha msingi wa kiimani kwa vijana.

Halikadhalika, Rais Dkt. Mwinyi amewahimiza waumini kuongeza juhudi katika ibada ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kuendeleza matendo ya huruma na ukarimu kwa wahitaji.

Katika mashindano hayo, Said Rashid Bakari kutoka Dar es Salaam ameibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha kuhifadhi Juzuu 30 na kutunukiwa shilingi milioni 5. Hafla hiyo pia ilihusisha utoaji wa Tuzo Maalum kwa heshima ya Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi, ambapo Rais Dkt. Mwinyi alipokea tuzo hiyo kwa niaba ya familia.

Hafla hiyo imehudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Mhe. Mama Mariam Mwinyi, viongozi wa dini, wadhamini na wananchi kwa ujumla.



Samia aahidi jeshi imara na la kisasa, azindua Makao Makuu ya Ulinzi ya Sh318.8 bilioni

Rais Samia Suluhu Hassan Jumanne alizindua rasmi Makao Makuu ya kudumu ya Ulinzi wa Taifa jijini Dodoma, akiahidi kuendelea kuwekeza ili kuhakikisha majeshi yanakuwa na vifaa vya kisasa, weledi na utayari wa kulinda usalama wa nchi.

Hafla hiyo iliyofanyika Kikombo, ilihudhuriwa na majenerali wa sasa na wastaafu, na kuambatana na shamrashamra za kijeshi. Tukio hilo limeelezwa na Rais kuwa hatua ya kihistoria katika kuimarisha usalama wa taifa na kuboresha miundombinu ya kijeshi.

Kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa Tanzania People's Defence Forces (JWTZ) mwaka 1964, Tanzania sasa ina makao makuu ya kitaifa ya ulinzi yaliyojengwa mahsusi ili kuimarisha amri, uratibu na ufanisi wa operesheni katika eneo moja.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Hassan alisisitiza umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya ulinzi wakati uchumi wa nchi ukiendelea kukua, akieleza uzinduzi huo kuwa hatua kubwa katika kuimarisha miundombinu ya ulinzi na ufanisi wa kiutawala ndani ya jeshi.

Alibainisha kuwa kukamilika kwa makao hayo kunatimiza ndoto ya muda mrefu iliyowahi kusisitizwa na Baba wa Taifa, Julius Nyerere, aliyetamani kuwepo kituo cha kudumu na cha kati cha amri ya ulinzi wa taifa.

"Ujenzi huu unalenga kuimarisha usalama wa nchi na kuongeza ufanisi wa taasisi zetu za ulinzi," alisema.

Rais aliongeza kuwa Tanzania ni miongoni mwa mataifa ya Afrika yanayotambua umuhimu wa sekta ya ulinzi kama nguzo ya kulinda mamlaka ya nchi na maendeleo. Alisisitiza kuwa taifa linalotaka kuheshimika kimataifa linapaswa kuwa na taasisi imara za ulinzi ili kulinda mipaka, rasilimali na wananchi wake.

Mbali na miundombinu, Rais alisisitiza maadili ya msingi ya jeshi imara, yakiwemo nidhamu, weledi, uaminifu na kuheshimu mamlaka ya kikatiba.

Makao hayo mapya yako umbali wa takribani kilomita 16.4 kutoka barabara kuu ya Dodoma–Morogoro, ndani ya eneo linalokua la mji wa serikali. Jengo hilo linahifadhi ofisi za JWTZ pamoja na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na kuunganisha shughuli zilizokuwa zikitawanyika katika maeneo mbalimbali.

Mradi huo ni sehemu ya mpango mpana wa kuhamisha taasisi kuu za serikali kwenda Dodoma, kuimarisha hadhi ya jiji hilo kama kitovu cha utawala wa nchi.

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, alisema awamu ya kwanza ya mradi imekamilika kwa gharama ya Sh121.49 bilioni na itaongeza ufanisi wa mifumo ya amri na uratibu wa vikosi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na JKT, Dk Faraji Mnyepe, alisema mradi mzima ulioanza Machi 10, 2020 utagharimu Sh318.8 bilioni na kutekelezwa kwa awamu tatu.

Na Ukhti Fatima SS
0713 420 780

Tuhoji uhalali wa nembo "Halal" au tuamini tu?

Waislamu wengi wanapoona alama ya "Halal" katika duka au mgahawa hukubali mara moja bila kuuliza maswali zaidi. Hata hivyo, makala iliyochapishwa na Muslim Network TV inaonya kuwa tabia hiyo inaweza kuwa hatari kwa sababu si kila bidhaa yenye alama hiyo huwa imethibitishwa ipasavyo.



Tuhoji uhalali wa nembo “Halal” au tuamini tu?



Waislamu wengi wanapoona alama ya “Halal” katika duka au mgahawa hukubali mara moja bila kuuliza maswali zaidi. Hata hivyo, makala iliyochapishwa na Muslim Network TV inaonya kuwa tabia hiyo inaweza kuwa hatari kwa sababu si kila bidhaa yenye alama hiyo huwa imethibitishwa ipasavyo.

Makala hiyo inaeleza kuwa katika Uislamu jukumu la kuhakikisha chakula ni halali si la mtu mwingine bali la Mwislamu mwenyewe. Mara nyingi watu huamua kutohoji kwa sababu wanaona Waislamu wengine wanakula hapo au wanaogopa kuonekana kana kwamba wanajiona bora zaidi kidini. Lakini ukweli ni kwamba kufuata sheria za chakula ni wajibu wa kila mtu binafsi.

Chanzo hicho kinaeleza pia kuwa soko la bidhaa za Halal duniani linaongezeka kwa kasi kubwa na linatarajiwa kufikia takribani dola trilioni 6 ifikapo mwaka 2034. Kutokana na fursa hiyo, biashara nyingi—ikiwemo zinazomilikiwa na wasiokuwa Waislamu—zinaingia katika soko hilo ili kupata faida. Wakati mwingine biashara hizo zinaweza kutumia neno “Halal” kama mbinu ya kuvutia wateja bila kufuata kikamilifu misingi ya Kiislamu.

Makala hiyo pia inapinga dhana potofu kuwa Halal inahusu nyama pekee. Kwa mujibu wa ufafanuzi wake, Halal inahusisha mfumo mzima wa uzalishaji kuanzia viambato, namna mnyama alivyochinjwa, usindikaji, uhifadhi, hadi usafirishaji wa bidhaa. Hata vitu vidogo kama vimiminika vya ladha, rangi za chakula, au kemikali za kutengeneza bidhaa vinapaswa kuwa halali.

Aidha, si kila chakula cha mboga au kinachoonekana “safi” kinakuwa Halal. Baadhi ya bidhaa zinaweza kuwa na gelatin, vimeng’enya au viungo vilivyotokana na vyanzo visivyo halali. Hivyo, uangalizi wa kina unahitajika kabla ya kuamini bidhaa yoyote.

Chanzo hicho pia kinaonya kuhusu uwezekano wa udanganyifu katika vyeti vya Halal. Baadhi ya wafanyabiashara huweka vyeti vya zamani, visivyo halali au vinavyoonyesha sehemu ndogo tu ya bidhaa zao. Kwa sababu hiyo, Halal haipaswi kuchukuliwa kama lebo rahisi kwenye pakiti bali ni mfumo unaohitaji uwajibikaji na ufuatiliaji wa mara kwa mara.

Hali hii inafungua mjadala muhimu pia kwa nchi kama Tanzania. Katika miji mingi, hasa maeneo ya biashara na vituo vya usafiri, watu hununua kuku wa kukaanga, mishkaki au nyama choma kwenye vibanda vya chipsi bila hata kujua nyama hiyo imetoka wapi au imechinjwa vipi.

Mara nyingi wauzaji hawa hawana vyeti vya Halal, na wateja wengi hawaulizi maswali. Wengine hata hawawajui wauzaji hao wala utaratibu wao wa kuchinja. Kwa kuzingatia kuwa Tanzania ina watu kutoka tamaduni na mitazamo tofauti kuhusu uchinjaji wa wanyama, suala hili linahitaji tahadhari zaidi kutoka kwa Waislamu wanaotaka kufuata misingi ya dini yao.

Hivyo, kama inavyosisitiza Muslim Network TV, uangalizi, elimu na uwajibikaji wa mtu binafsi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa kile tunachokula kinaendana na mafundisho ya Kiislamu.

NA MWANDISHI WETU

Z'bar yafungua ushirikiano mpya wa kikanda kupambana na uvuvi haramu

$142m

Nchini Tanzania pekee, hasara zinazohusishwa na IUUF zilikadiriwa kufikia dola milioni 142.8 kwa mwaka kati ya 2015 na 2021, zikichangiwa zaidi na uvunaji haramu wa kamba na jodari.

Nchi za Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi zimeahidi kuimarisha ushirikiano katika kupambana na uvuvi haramu, usioripotiwa na usiodhibitiwa (IUUF), hatua ambayo maafisa wanasema inaashiria mabadiliko kutoka mijadala ya kiufundi iliyotawanyika kwenda kwenye mwitikio wa pamoja wa kikanda.

Ahadi hiyo ilirasimishwa mwezi uliopita visiwani Zanzibar kupitia kusainiwa kwa Mkataba wa Maazimio na Mapendekezo chini ya Mradi wa Jahazi. Hafla hiyo iliwaleta pamoja wawakilishi kutoka Tanzania Bara, Zanzibar na Kenya, huku Mauritius, Msumbiji, Comoro, Ushelisheli na Madagascar pia zikishiriki.

Kwa miongo kadhaa, IUUF katika ukanda huo ilichukuliwa zaidi kama suala la udhibiti na utekelezaji ndani ya majukwaa ya usimamizi wa uvuvi na ripoti za ufuatiliaji. Hata hivyo, katika ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki wenye urefu wa kilomita 4,600, athari zimekuwa kubwa: kupungua kwa samaki, kushuka kwa kipato na kuongezeka kwa shinikizo kwa zaidi ya watu milioni tatu wanaotegemea uvuvi kwa maisha yao.

Uvuvi wa pwani huzalisha zaidi ya tani milioni 1.5 za samaki kwa mwaka, ukiwa nguzo muhimu ya usalama wa chakula na uthabiti wa uchumi. Hata hivyo, wadau wanaonya kuwa nguzo hiyo iko chini ya tishio la kudumu, huku ukanda ukikadiriwa kupoteza takribani dola milioni 415 kila mwaka kutokana na uvuvi haramu. Meli za uvuvi za mbali zinazoungwa mkono na serikali zimetuhumiwa kuvua kupita kiasi, kuharibu mazalia na kutupa baharini samaki wasiokusudiwa.

Nchini Tanzania pekee, hasara zinazohusishwa na IUUF zilikadiriwa kufikia dola milioni 142.8 kwa mwaka kati ya 2015 na 2021, zikichangiwa zaidi na uvunaji haramu wa kamba na jodari. Nchi hiyo inashika nafasi ya 82 duniani kwa kiwango cha hatari ya IUUF. Kenya nayo inakabiliwa na changamoto kama hiyo, ambapo uvuvi haramu unakadiriwa kuchangia kati ya asilimia 30 na 40 ya samaki wote wanaovuliwa.

Zanzibar, ambako uchumi wa buluu unaajiri takribani theluthi moja ya wananchi, inakabiliwa na athari kubwa. Kwa ujumla nchini Tanzania, kupungua kwa samaki karibu na fukwe kumesababisha takribani asilimia 75 ya wavuvi kuelekea bahari kuu, hali inayoongeza gharama na hatari kwa wavuvi wadogo.

Mataifa ya visiwa kama Mauritius na Ushelisheli, yanayotegemea uvuvi wa jodari na mauzo ya mazao ya baharini, pia yanapoteza mapato kutokana na uvuvi haramu na utoaji taarifa pungufu. Nchini Msumbiji, Madagascar na Comoro, ambako uvuvi wa pwani ni tegemeo la ajira na lishe, uvunaji haramu unaongeza hatari kwa jamii zilizo tayari kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania imesema ingawa teknolojia za ufuatiliaji kama mifumo ya kufuatilia meli na satelaiti zimeboreshwa, mafanikio hayo hayawezi kuziba mapengo ya mifumo ya sheria na utekelezaji isiyounganishwa.

Wadau wamebainisha changamoto zikiwemo tofauti za usajili wa meli, viwango visivyolingana vya adhabu na ukosefu wa kubadilishana taarifa kwa wakati, hali inayowawezesha wahalifu kutumia mianya ya mipaka ya bahari.

Maafisa wa sekta ya uvuvi wamesisitiza kuwa IUUF si suala la rasilimali pekee, bali pia ni changamoto ya maendeleo ya binadamu inayogusa usalama wa chakula, kipato cha kaya na mustakabali wa uchumi.

Katika mkutano wa kikanda wa Blue Voices uliofanyika Zanzibar, serikali, wataalamu wa sheria, mamlaka za bandari, watafiti na asasi za kiraia walikutana kuweka mkakati wa pamoja wa kukabiliana na tatizo hilo.

NA MUGINI SINGIRA

Zanzibar yadhamiria kupunguza utegemezi kwa wafadhili

Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Juma Maliki Akili, amesema mpango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kukopa na kulipa madeni kwa kutumia rasilimali zilizopo nchini na siyo kusubiri fedha za misaada ambazo wakati mwingine huchelewa.

Waziri Juma aliyasema hayo wiki iliyopita wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar na kusisitiza kuwa wawekezaji katika viwanda na sekta ya utalii wataweza kupata huduma bora za kibenki ambazo pia zitafanikisha kutekeleza miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

“Tunakuza uchumi kupitia shughuli za uwekezaji ujenzi na za kifedha, shughuli hizi zimechachua sana uchumi wa wananchi na kusaidia kuondoa tatizo la ajira pamoja na kwamba bado lipo kwa kiasi. Nitoe wito kupitia tawi jipya la benki ya KCB tuzingatie sana kutengeneza pia ajira kwa vijana wenye taaluma na wanakosa nafasi hizo,” alisema Waziri Juma. Naye Mwenyekiti wa Bodi ya benki ya KCB, Balozi Peter Kallaghe, alisema hatua ya kuweka tawi la benki hiyo Zanzibar inaakisi dhamira ya kukuza uchumi jumuishi, kuharakisha mageuzi ya sekta ya fedha, kuendeleza uchumi wa buluu, kuiwezesha sekta binafsi na kutumia teknolojia kama kichocheo cha maendeleo ya kifedha na jamii.

UKHTI FATIMA SS

Sheikh Ibrahim aonya mitego ya kuwaondoa Waislamu katika ibada

Mhadhiri Sheikh Ibrahim Twaha Ibrahim ametanabaisha kuwa makafiri wameweka mitego mingi ya kuwaondoa katika ibada nwezi huu wa Ramadhan, na hivyo kuwataka Waislamu kuwa waangalifu.

Sheikh Ibrahim aliyasema hayo katika khutba ya Sala ya Ijumaa katika Msikiti wa Haqq mjini Morogoro, ambapo mada yake ilihusu Fadhila za Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

"Tunafahamu makafiri wamepanga mipango mingi sana. Mechi hizi kubwakubwa wameziweka ndani ya Ramadhan. Mnasali tarawehe, huku mechi inaendelea. Hivyo mtu anatoka, haswali tarewehe anakimbilia mechi. Laa msifanye hivyo," alieleza Sheikh Twaha.

Sheikh Ibrahim ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya The Islamic Foundation, pia amewaasa Waislamu nchini kujikita katika kufanya ibada katika mwezi wa Ramadhan ambao una fadhila nyingi na kubwa.

Aidha, Sheikh Ibrahim amewaasa Waislamu kepuka kutumia mwezi wa Ramadhan kwa kufanya maasi, ikiwemo kuandaa ligi za michezo maalum kwa jina la mwezi huo mtukufu.

> **"Tunafahamu makafiri wamepanga mipango mingi sana. Mechi hizi kubwakubwa wameziweka ndani ya Ramadhan. Mnasali tarawehe, huku mechi inaendelea. Hivyo mtu anatoka, haswali tarewehe anakimbilia mechi. Laa msifanye hivyo"**
>
> **Sheikh Ibrahim Twaha**

Katika khutba yake, Sheikh Ibrahim alielezea faida mbalimbali za mwezi huo ikiwa ni pamoja na kusamehewa dhambi na kuandikiwa Pepo.

Miongoni mwa ibada alizohimiza watu kufanya kwa wingi ni kusoma Qur'an, kutoa sadaka pamoja na sala za Sunna, ambapo kipekee alihimiza watu wasali tarawehe na witri hadi mwisho nyuma ya imam ili waandikiwe kisimamo cha siku nzima, kwa mujibu wa hadith ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

"Wanazuoni wanasema, kisimamo cha tarawehe katika mwezi wa Ramadhan ndio kisimamo cha Tahajjud katika miezi mingine. Mwezi wa Ramadhan ikaitwa tarawehe, miezi mingine ikaitwa Tahajjud," alisema Sheikh Ibrahim.

Akifafanua hadith husika iliyosimuliwa Abu Huraira kuhusu tarawehe nyuma ya imam, alisema: "Mmeswali swala ya Isha, kisha ukasimama na imamu mpaka mkamaliza kusali na tarawehe... hadi witri, basi umeandikiwa kisimamo cha usiku mzima."

Kisha akahoji haraka inayooneshwa na baadhi ya Waislamu kuacha njiani: "Kwa nini unajisumbua ukifika rakaa nane unaondoka? Maliza na imam ili uandikiwe kisimamo cha usiku mzima."

Hata hivyo, Sheikh Ibrahim alisema haikatazwi mtu kundelea na sala zake nyingine baada ya kumaliza tarawehe na imam.

"Na hakuna ubaya wewe ukasimama na Imam halafu baadae usimame tena uswali swala zako... lakini kwanza andikiwa kisimamo cha usiku mzima pamoja na imam."

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

Sote tunafahamu kwamba kusoma Qur'an Tukufu ni kitendo kikubwa cha ibada. Usomaji wa Qur'an kwa sauti nzuri ya kuvutia (melodious) hutuliza moyo. Lakini je, hiyo inatosha? Hebu fikiria mtu anaanza safari ndefu kupitia jangwa lenye joto kali na kisha misitu minene. Amepewa ramani nzuri na sahihi zaidi kuwahi kutengenezwa hapa duniani.



Tusome Qur'an kwa kuzingatia maana yake

Tusome Qur’an kwa kuzingatia maana yake

Sote tunafahamu kwamba kusoma Qur’an Tukufu ni kitendo kikubwa cha ibada. Usomaji wa Qur’an kwa sauti nzuri ya kuvutia (melodious) hutuliza moyo. Lakini je, hiyo inatosha? Hebu fikiria mtu anaanza safari ndefu kupitia jangwa lenye joto kali na kisha misitu minene. Amepewa ramani nzuri na sahihi zaidi kuwahi kutengenezwa hapa duniani.

Kila jioni, anafungua ramani yake, anaibusu, anafuata mistari yake kwa mshangao, lakini hasomi muongozo wake hata mmoja. Anatangatanga bila malengo kwa miaka mingi bila kutambua kwamba anakoelekea kulikuwa jirani kabisa, na alibakisha siku moja tu kufika!

Wakati mwingine, inaonekana tunaichukulia Qur’an kama msafiri huyu aliyepotea, tukipuuza maana ya maneno tunayosoma na kutotumia fursa ya ujumbe tuliopewa na Muumba wa Mbingu na Ardhi.

Allah ‘Azza Wajallah’ anatahadharisha ndani ya Qur’an: “Je! Hawaizingatii hii Qur’an? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?” [Qur’an, 47:24]. Aya hii inaweka wazi kwamba kusoma Qur’an tu bila kuelewa maana yake haitoshi.

Hebu fikiria mtu baki tu aliyesimama na kukutazama akisema “Kwanini urudie maneno ambayo huyaelewi?”, au akisema, “Kama kitabu hiki ni muongozo, kwanini hujaribu kujua kinasema nini?”

Kuisoma Qur’an kwa qiraa sahihi ni jambo zuri, lakini kuielewa Qur’an huleta mabadiliko. Hakuna njia bora zaidi ya kufungua nguvu hiyo ya mabadiliko kuliko kusikiliza tafsiri za sauti zilizo wazi katika lugha mbalimbali. Waislamu wa awali hawakutenganisha ibada kutoka kwenye mawazo.

Fikiria kauli iliyotajwa sana ya sahaba Abu al–Darda (Allah amridhie): “Kutafakari kwa saa moja ni bora zaidi kuliko kusimama usiku kucha katika sala.” Kutafakari si kinyume cha sala ya usiku, bali ndiko hufanya kila tendo la ibada liwe hai.

Hebu fikiria jinsi sala yako ya tarawehe inavyohuishwa pale unapoelewa kinachosomwa kutoka ndani ya Qur’an usiku huo! Kikwazo kwa wengi wetu ni kutoifahamu vyema lugha ya Kiarabu.

Ili kutusaidia katika safari yetu ya kufungua tabia hii ya Qur’an ya kuleta mabadiliko, unaweza kusikiliza tafsiri ya Qur’an kwa lugha ya Kiswahili iliyorekodiwa kwa ubora wa hali ya juu, ambayo huleta maana ya Qur’an katika maisha kwa njia iliyo wazi na jumuishi.

Sikiliza tafsiri ya Qur’an ukiwa njiani kwenda kazini, ukiwa na familia yako, au ukiwa katika chumba tulivu, na jizamishe katika ujumbe wa ajabu kutoka kwa Mola wako ulioletwa na malaika Jibril na kuwasilishwa na Nabii wa mwisho kwa wanadamu, Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie).

Utayarishaji huu wa kipekee (production) huleta kina na uwazi wa ujumbe wa Qur’an, na kutoa uzoefu wenye nguvu unaoweza kusikilizwa na Waislamu na wasio Waislamu pia.

Simulizi ya kitaalamu iliyowekwa sauti (narration) na mbobezi katika istilahi za Kiislamu, rekodi hii inahakikisha kwamba uzuri na maana ya Qur’an Tukufu inawasilishwa kwa usahihi na heshima. Unaweza kusoma tafsiri nzima kwa saa 15 tu!

Kiukweli, kwa kusikiliza dakika 30 kila siku, utaweza kusoma maana nzima ya Qur’an kwa mwezi mmoja tu! Unasubiri nini? “Na hiki Kitabu tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya zake, na wawaidhike wale wenye akili.” [Qur’an, 38:29].

رمضان

SEHEMU YA 2

MAKALA YA AFYA

0764 101 018

DKT.
Omar A. Kasuwi
Daktari Bingwa Mshauri wa magonjwa Moyo!
Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA)

Faida ya amadhani (Swawm) kwa msingi wa sayansi na Uisilamu wenyewe.!

Mtume alisema:

"Funga ni kinga."

(Bukhari) Usumbufu huu ni sehemu ya mafunzo ya subira.

Matengenezo ya Seli Na Kinga ya mwili (Autophagy-self cleansing)!

Kufunga huanzisha mifumo ya ndani ya matengenezo kama- Usafishaji wa seli zilizochoka (autophagy -self cleansing) ,Uboresha mitochondria, kupunguza uchochezi mwilini na kuimarisha ulinzi wa mwili.

Kiroho, hili linafanana na utakaso wa nafsi — kuacha tabia mbaya kama mwili unavyoondoa vitu vilivyoharibika.

Kuimarika kwa Afya ya Ubongo na Hali ya Kisaikolojia -Wakati wa kufunga, mwili huzalisha (ketoni) zinazochochea BDNF: ambazo huboresha ufanyaji kazi wa ubongo,kumbukumbu, hulinda ubongo na huongeza utulivu wa akili. Waislamu wenye kujaaliwa kufunga Ramadhani kwa Nia na ubora wake Wengi huhisi utulivu zaidi mara baada ya ramadhani kumalizika .

Mtume alisema:-

"Akifunga mmoja wenu asiwe mchafu wa maneno wala hasira; akichokozwa aseme: Mimi nimefunga."

(Bukhari na Muslim)-Hii ni mafunzo ya kudhibiti hisia jambo linalotambulika kisayansi kama udhibiti wa ubongo wa mbele (prefrontal control).Kufunga Ramadhani haiathiri tu kimetaboliki bali pia huathiri hisia na fikra.Tafiti za Ramadhani zinaonyesha:,kuongezeka kwa ubora wa maisha, kupungua kwa msongo na huzuni. Ketoni hutoa nishati thabiti kwa ubongo, ndiyo maana watu wengi huhisi akili kuwa wazi zaidi katikati ya Ramadhani.

Kupungua kwa Uzito na Mafuta ya Tumbo!

Kufunga Ramadhani si lazima kupunguze uzito sana, lakini huboresha muundo wa mwili.Tafiti zinaonyesha:,kupungua kwa mafuta ya mwili,hupunguza uzito endapo tu tutafunga kwa nia na kufturu kwa nidhamu ya Afya.Muhimu zaidi ni kupungua kwa mafuta ya ndani ya tumbo (visceral fat) ambayo yanahusishwa sana na ugonjwa wa moyo na kansa.

Usawazishaji wa Homoni za Njaa!

Kufunga hubadilisha mabadiliko makubwa ya homoni za ghrelin , na leptin .Hali hii husababisha kupungua kwa homoni hizi hatimae kupunguza hamu ya kula na kupunguza kula bila mpangilio, Kadri Siku za Funga zinavoendelea mwili ndivo unavozidi kujiimarisha sehemu zote. Homoni hizi hupungua na kupunguza kuskia njaa na hamu ya kula pia ,pamoja na kwamba Mfungaji huendelea kujishughulisha na majukumu yake ya kila siku ya kujipatia rizki. Ndiyo maana mwishoni mwa Ramadhani mtu huwa haisi njaa kuliko mwanzoni.

Kutokunywa maji mchana husababisha upungufu mdogo wa maji kwa muda na mwili hujirekebisha kuhifadhi maji yanayozalishwa ndani, ili kuiweka hali ya damu katika usawa unaotarajiwa ,kwa kuzuia mkojo kipindi hiki cha kufunga,

Wakati wa kufungua -Njia bora:ni kuanza na Maji kiasi,Tende na baadae mle chakula laini kwanza, kwa kufuatiwa na kile kiasi laini kiasi kigumu. Si afya kuftari kwa wingi kwani kuna athiri afya zenu. Kwa ubora zaidi tuftari chakula chenye uwiano sahihi wa Protein, Wanga, mafuta na vitamini.

Mazoezi-Mazoezi mepesi baada ya futari husaidia mwili kutumia sukari vizuri na Mazoezi bora zaidi ni kutembea kwenda kuswali msikitini swala ya tarweh.

faida za funga kwa msingi wa Iman.!

Sayansi inaeleza jinsi kufunga kunavyosaidia mwili.

Uislamu unaeleza dhumuni lake."Enyi mlioamini! Mmefaradhishiwa kufunga kama walivyofaradhishiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mwenyezi Mungu."

(Qur'an 2:183)Hivyo lengo si njaa — ni taqwa, yaani ulinganifu wa Allah katika maisha yote.

Nidhamu ya tabia na kujidhibiti!

Mtume amesema:"Funga ni ngao."

(Bukhari na Muslim) Ngao dhidi ya:hasira,maneno mabaya,tabia mbaya

Na pia:"Asiyeacha kusema uongo na kuutenda, Mwenyezi Mungu hana haja na kuacha kwake chakula na kinywaji."

(Bukhari)Hivyo kufunga hubadilisha tabia, si tumbo pekee.

Msamaha na mwanzo mpya-"Atakayefunga Ramadhani kwa imani na kutaraji thawabu atasamehewa madhambi yake yaliyopita."

(Bukhari na Muslim)Ramadhani ni utakaso wa moyo kama mwili unavyosafishwa.

Ikhlasi-ibada ya siri-"Kila amali ya mwanaadamu ni yake isipokuwa kufunga — ni Yangu nami ndiye ninalipa."

(Hadith Qudsi)-Hakuna ajuaye umefunga isipokuwa Mwenyezi Mungu — hapa ndipo ukweli wa ndani hujengwa.

Huruma , Unyenyekevu ,sadaka na shukrani!

Njaa humfanya mtu atambue wenye huhitaji kwani inamkumbusha ile hali ya wale wenye kukosa kila siku katika maisha yetu.

"...ili mpate kushukuru."

(Qur'an 2:185)Kukosa kwa muda hufundisha kuthamini ulichonacho.

Hitimisho!

Funga Ramadhani si ibada pekee

MAHMOUD NYAMGUMA

Muslim Charity, IOM wapeleka faraja Gaza wakati wa Ramadhan

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) likishikiana na Shirika la Hisani la Kiislamu la Muslim Charity wameelekeza msaada wa dharura kwa familia za Kipalestina katika Ukanda wa Gaza wakati Waislamu duniani wanaanza mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Kwa mujibu wa taarifa ya IOM iliyochapwa katika tovuti yake, maelfu ya wakazi wa Gaza wanalazimika kuadhimisha Ramadhan wakiwa katika mahema ya dharura baada ya kupoteza makazi yao kufuatia vita vilivyoendelea katika eneo hilo.

Kupitia ushirikiano kati ya IOM na taasisi ya Muslim Charity, mahema 448 ya dharura yamenunuliwa kwa gharama ya dola 300,000 ili kusaidia takribani watu 2,464 waliokosa makazi.

Msaada huo unalenga kuwapatia hifadhi ya muda familia ambazo zimeathiriwa vibaya na mgogoro huo huku mahitaji ya kibinadamu yakiendelea kuongezeka. IOM imesema pia inaendelea kusambaza vifaa muhimu kwa familia zilizo katika mazingira magumu zaidi.

Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa, karibu wakazi wote wa Ukanda wa Gaza wapatao zaidi ya milioni mbili wameathiriwa kwa namna moja au nyingine na vita, huku wengi wakilazimika kuhama makazi yao mara kadhaa.

Ripoti za mashirika ya kibinadamu zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya miundombinu ya makazi imeharibiwa au kuathiriwa vibaya, hali inayowaacha maelfu ya familia wakiishi katika makazi ya muda na maeneo yenye msongamano mkubwa.

IOM imeeleza kuwa katika miezi ya karibuni imesambaza zaidi ya vifaa vya msaada milioni 1.77, vikiwemo mahema zaidi ya 28,000 na blanketi 340,000. Hata hivyo, mahitaji bado ni makubwa kutokana na kiwango kikubwa cha uharibifu wa makazi na miundombinu mingine.

Mfuko wa Kiislamu wa IOM ulioanzishwa mwaka 2025 umechangisha zaidi ya dola milioni 2.6 kusaidia juhudi za makazi ya dharura Gaza, huku mashirika ya misaada yakisema msaada wa kimataifa unaendelea kuwa muhimu hasa katika kipindi cha Ramadhan.

Makazi salama ni haki ya msingi inayotambuliwa kimataifa. Hali ya Gaza inazua mjadala mpana kuhusu wajibu wa jumuiya ya kimataifa kulinda raia wakati wa migogoro.

Swali linalobaki ni je, dunia itaridhika kuona Ramadhan ya Wapalestina ikiendelea kuwa ya mahema na mateso, au itachukua hatua za kudumu kurejesha maisha ya kawaida na kuheshimu haki zao za msingi kama binadamu.

HABARI KIMATAIFA

MAHMOUD NYAMGUMA

Dubai vipimo vya afya bure mwezi mzima wa Ramadhan

Dubai imeanzisha mpango maalumu wa kutoa vipimo vya afya bila malipo katika baadhi ya bustani maarufu za jiji hilo wakati wa mwezi wa Ramadhan. Lengo la mpango huo ni kuhamasisha wananchi kufanya uchunguzi wa mapema wa magonjwa na kukuza utamaduni wa kujali afya.

Mpango huo utaendeshwa kupitia mabasi maalumu ya huduma za afya yatakayozunguka maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko mikubwa ya watu. Hatua hiyo inalenga kuwafikia wakazi wengi zaidi, hasa wakati wa Ramadhan ambapo familia hukutana katika bustani na maeneo ya wazi kabla ya kufuturu.

Kwa mujibu wa Idara ya Masuala ya Kiislamu na Shughuli za Hisani ya Dubai, mpango huo ni sehemu ya kampeni ya Ramadhan iitwayo "Step of Life." Huduma hizo zitatolewa kwa ushirikiano na taasisi za afya za Prime Medical Care pamoja na Noor Dubai Foundation. Huduma zitakazotolewa ni pamoja na uchunguzi wa macho, vipimo vya shinikizo la damu na kiwango cha sukari mwilini. Vipimo hivi vinalenga kugundua mapema magonjwa sugu na kuwahamasisha watu kubadili mtindo wa maisha ili kuimarisha afya zao.

Mbali na kutoa vipimo, wahudumu wa afya pia watatoa elimu kuhusu namna ya kuzuia magonjwa na umuhimu wa kufuatilia afya mara kwa mara.

Hamas yarejesha udhibiti Gaza, vikwazo tele kuelekea amani

Harakati ya Kiislamu ya Hamas imethibitisha kurejesha udhibiti katika maeneo makubwa ya Ukanda wa Gaza yaliyokuwa yameachwa na jeshi la Israel kufuatia makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyosaidiwa na upatanishi wa kimataifa.

Vikosi vya polisi vinavyohusishwa na harakati hiyo vimeonekana kurejea mitaani kusimamia usalama, kuratibu shughuli za kila siku na kusaidia kurejesha huduma za msingi katika baadhi ya miji ya Gaza.

Hatua hiyo imekuja wakati wakazi wa Gaza wakikabiliana na hali ngumu ya kibinadamu baada ya vita vilivyodumu kwa muda mrefu. Sehemu kubwa ya miundombinu imeharibiwa na idadi kubwa ya wananchi wanategemea misaada ya chakula. Katika mazingira hayo, kurejea kwa utaratibu wa usalama mitaani kumeonekana kuwa muhimu kwa kuendeleza shughuli za kijamii na kiuchumi.

Wakati huo huo, Hamas imetoa msimamo wake kuhusu mpango wa kimataifa unaojadiliwa wa kupeleka kikosi cha kulinda amani Gaza.

Msemaji wa harakati hiyo Hazem Qassem amesema wako tayari kukubali uwepo wa vikosi vya kimataifa vitakavyosimamia usitishaji wa mapigano na kuwa kizuizi kati ya jeshi la Israel na raia wa Gaza. Hata hivyo alisisitiza kuwa vikosi hivyo havipaswi kuingilia mambo ya ndani ya eneo hilo.

Kauli hiyo imekuja baada ya mkutano wa kile kinachoitwa "Board of Peace" ulioandaliwa nchini Marekani, ambapo baadhi ya nchi ziliahidi kuchangia askari katika kikosi kipya cha kimataifa cha utulivu. Mpango huo ni sehemu ya juhudi za kidiplomasia zinazolenga kuimarisha usalama na kusaidia mpito wa kisiasa baada ya vita.

Hata hivyo, juhudi hizo za amani zinaonekana kukabiliwa na changamoto kubwa kutokana na kauli na sera kutoka upande wa serikali ya Israel. Waziri wa fedha wa Israel mwenye msimamo mkali Bezalel Smotrich amesema anataka kuhimiza "uhamiaji" wa Wapalestina kutoka Gaza na Ukingo wa Magharibi huku akipendekeza kufutwa kwa makubaliano ya Oslo.

Wakati matamshi hayo yakikosolewa kimataifa, hali halisi katika Ukingo wa Magharibi inaendelea kuzua wasiwasi. Ripoti zinaonyesha kuongezeka kwa mashambulizi ya walowezi wa Kiyahudi dhidi ya vijiji vya Kipalestina pamoja na uvamizi wa ardhi za wakulima.

Katika baadhi ya maeneo karibu na Ramallah, wakazi wanasema hawawezi tena kufika kwenye mashamba yao kutokana na vitisho na uwepo wa wanajeshi.

Waislamu wengi Nigeria hatarini kukosa Hija 2026

Maelfu ya Waislamu nchini Nigeria wako katika hatari ya kukosa ibada ya Hija ya mwaka 2026 baada ya mfumo wa usajili wa Saudi Arabia kufungwa kabla wengi hawajakamilisha taratibu zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Ijumaa na Naibu Mkurugenzi wa Habari na Machapisho wa Tume ya Hija ya Nigeria (NAHCON), Fatima Usara, changamoto hiyo imetokana na kuchelewa kwa tangazo la kuongezwa kwa idadi ya mahujaji waliotengewa Nigeria.

Awali, mamlaka za Saudi Arabia zilipunguza idadi ya mahujaji wa Nigeria kutoka 95,000 hadi 50,000. Hata hivyo, baada ya juhudi za kidiplomasia, nafasi zaidi ziliidhinishwa baadaye, lakini tangazo hilo lilitolewa baada ya dirisha la usajili kufungwa. NAHCON ilieleza kuwa ililazimika kutumia utaratibu wa "aliyewahi kulipa kwanza ndiye kuhudumiwa kwanza." Baadhi ya majimbo yalifanikiwa kukamilisha malipo na maandalizi kabla ya tarehe ya mwisho ya Januari 2.

Tume hiyo imeonya kuwa mamlaka za Saudi Arabia huzingatia sana muda wa mwisho wa usajili, hivyo waliochelewa wanaweza kukosa safari hiyo muhimu ya ibada. Waliolipa kuchelewa wametakiwa kuwa watulivu huku hatua za kutafuta suluhisho zikiendelea.

Soko la vipodozi vya Halal lakua kwa kasi duniani

Soko la kimataifa la vipodozi vinavyokidhi viwango vya Kiislamu linaendelea kukua kwa kasi, huku wataalamu wakitabiri ongezeko kubwa la thamani ya biashara hiyo katika miaka ijayo. Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa na Market Research Industry Today, soko la vipodozi vya Halal linaweza kufikia dola za Marekani bilioni 15 ifikapo mwaka 2035, kutoka takribani dola bilioni 4.96 mwaka 2024.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa ukuaji huo unatarajiwa kuwa wastani wa asilimia 10.6 kila mwaka kati ya 2025 na 2035. Ongezeko hilo linachangiwa na kukua kwa idadi ya Waislamu duniani pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa watumiaji kuhusu bidhaa zinazozingatia misingi ya Kiislamu.

Bidhaa za vipodozi vya Halal hujumuisha bidhaa za ngozi, vipodozi na huduma za nywele ambazo hazina pombe, viambato vinavyotokana na nguruwe au kemikali zisizokubalika kidini. Wataalamu wanasema vijana wengi wa Kiislamu sasa wanapendelea bidhaa safi zenye viambato vya asili.

Wakati huohuo, uchambuzi uliotolewa na Vocal Media unaonyesha kuwa soko hilo linaongezeka kwa kasi hata katika nchi binafsi. Nchini Saudi Arabia, soko la vipodozi vya Halal linatarajiwa kuongezeka kutoka dola bilioni 3.57 mwaka 2024 hadi zaidi ya dola bilioni 11.16 ifikapo 2033.

Wachambuzi wanasema ukuaji huo pia unasukumwa na biashara za mtandaoni, ushawishi wa mitandao ya kijamii na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa salama na zenye maadili. Leo, vipodozi vya Halal havilengi Waislamu pekee bali pia watumiaji wanaotafuta ubora na uwazi katika bidhaa za urembo.

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

Benki za Kiislamu zapanua sehemu ya soko Uturuki

Sehemu ya soko inayoshikiliwa na benki za Kiislamu nchini Türkiye imeongezeka hadi asilimia 9.2 mwaka 2025 kutoka asilimia 8.1 mwaka 2024, kulingana na ripoti mpya ya Fitch Ratings iliyoripotiwa na Arab News. Ripoti hiyo inaonyesha kuwa ukuaji huo umechangiwa na kuongezeka kwa huduma za mikopo (financing) na amana (deposits) katika benki hizo kwa kasi zaidi kuliko sekta nzima ya benki. Sehemu ya soko ya ufadhili ilifikia asilimia 7.9 mwaka 2025 kutoka asilimia 7.3 mwaka uliotangulia, huku amana zikifikia asilimia 10.4 kutoka asilimia 9.4.

Fitch Ratings imeeleza kuwa kuanzishwa kwa benki mpya za Kiislamu, hasa zile za kidijitali, kunachochea ukuaji huo. Uwekezaji kutoka nchi za Baraza la Ushirikiano la Ghuba (GCC) pia unatarajiwa kuendelea kuimarisha sekta hiyo.

Mahusiano ya karibu ya Türkiye na nchi za Kiislamu katika Balkans, Afrika na Mashariki ya Kati pia yanatajwa kusaidia kuvutia wawekezaji zaidi katika sekta ya fedha za Kiislamu. Ripoti hiyo inatabiri kuwa sehemu ya soko ya benki za Kiislamu itaendelea kuongezeka mwaka 2026, ingawa changamoto kama mfumuko wa bei na mikopo yenye hatari zinaweza kuongeza kiwango cha mikopo chechefu kidogo. Hata hivyo, kiwango hicho bado kiko chini ya wastani wa sekta nzima ya benki nchini humo.

Umrah kusitishwa mapema kupisha maandalizi ya Hija 2026

Serikali ya Saudi Arabia imetangaza kusitisha kwa muda ibada ya Umrah kabla ya kuanza maandalizi ya msimu wa Hija wa mwaka 2026. Hatua hiyo imetangazwa na Wizara ya Hija na Umarh ikiwa ni sehemu ya kupanga vizuri shughuli za ibada hiyo kubwa ya Kiislamu.

Kwa mujibu wa ratiba rasmi iliyotolewa, Machi 19, 2026 itakuwa siku ya mwisho kutuma maombi ya visa ya Umrah. Aidha, Aprili 2, 2026 ndiyo itakuwa tarehe ya mwisho kwa mahujaji wa kigeni kuingia nchini humo.

Mamlaka hizo pia zimeeleza kuwa mahujaji wote waliopo nchini humo kwa ajili ya Umrah wanapaswa kuondoka kabla au ifikapo Aprili 18, 2026. Baada ya tarehe hiyo, ibada ya Umrah itasimamishwa kwa muda ili kutoa nafasi kwa maandalizi ya msimu wa Hija.

Wizara hiyo imesisitiza kuwa hatua hizo ni za kawaida kila mwaka na zinalenga kuhakikisha maandalizi ya Hija yanafanyika kwa usalama, utaratibu na ufanisi mkubwa.

Waislamu wanaopanga kufanya Umrah wameshauriwa kupanga safari zao mapema, kuzingatia tarehe zilizotolewa na kuhakikisha wanazingatia masharti ya visa ili kuepuka adhabu au usumbufu wa safari. Huduma za Umrah zinatarajiwa kurejea tena baada ya kumalizika kwa ibada ya Hija.

Kenya yakiri mpango wa kuuza nyama Ghuba kusuasua

Serikali ya Kenya imekiri kuwa mpango wake wa kusafirisha nyama na bidhaa zake katika nchi za Ghuba haujatekelezwa kama ilivyotarajiwa, licha ya kuwepo kwa soko lenye mahitaji makubwa katika eneo hilo.

Maafisa wa serikali, wakinukuliwa na gazeti la Busines Daily, walisema tathmini ya katikati ya mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia imeonyesha kuwa utekelezaji umechelewa, jambo lililosababisha fursa za biashara katika soko la Ghuba kutotumika ipasavyo.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa tafiti za soko zimeonyesha kuwa kuna mahitaji ya kudumu ya nyama nyekundu yenye cheti cha halal katika nchi kama United Arab Emirates na Saudi Arabia. Hata hivyo, changamoto katika uzalishaji, ubora na usafirishaji zimekuwa kikwazo.

Sasa serikali inapanga kuandaa mkakati mpya wa kuboresha mnyororo wa thamani wa sekta ya mifugo, ikiwemo kuimarisha uzalishaji, kufikia viwango vya kimataifa na kutumia teknolojia katika utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo.

Hatua hizo zinatarajiwa kusaidia Kenya kunufaika na soko kubwa la nyama katika eneo la Ghuba.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

Kufunga tu haitoshi, tushindane kufanya mema

Ramadhan ni mwezi uliosheheni ibada mbalimbali, ni gulio la kila heri, na ni msimu wa kupata faida kwa kila ibada. Katika mwezi huu Mtukufu, Waumini hupata fursa ya kujikurubisha kwa Muumba wao ili kupata radhi zake na hatimaye kulipwa Pepo siku ya Kiyama. Kwa minajili hiyo, tunapaswa kuupokea mwezi wa Ramadhan kwa uzito unaostahiki. Tusipoupa mwezi wa Ramadhan uzito wake unaostahili, tutakuwa tumeshindwa kutambua tofauti ya mwezi huu na miezi mingine katika ubora na fadhila zake na hivyo kutufanya tushindwe kujipinda katika kuchuma heri za msimu huu.

Ni mwezi wa kushindana katika heri

Katika Qur'an tukufu, Allah anatutaka tushindane na kuharakia heri kwa kusema: "Na kila mmoja anao upande anaoelekea. Basi shindanieni mema. Popote mlipo Mwenyezi Mungu atakuleteni nyote pamoja. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu." [Qur'an, 2:148].

Katika aya nyingine, Allah Aliyetukuka anasema: "Na yakimbilieni Maghfira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni (sawa na) mbingu na ardhi, iliyowekwa tayari kwa wachamungu." [Qur'an, 3:133]. Pia Allah amesema: "Na katika hayo washindanie wenye kushindana." [Qur'an, 83:26].

Katika aya hizo na nyingine nyingi mfano wake, Allah anatutaka tuwe ni wenye kushindana na kwenda mbio katika mambo yote ya heri, kama alivyowasifia Mitume wake kwa sifa hii aliposema: "Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na wakituomba kwa shauku na hofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea." [Qur'an, 21:90].

Masahaba (Allah awaridhie wote) walikuwa na wivu katika mambo ya heri pale walipohisi kuwa wanazidiana. Kila mmoja alipenda amzidi mwenzake. Hili linaonekana wazi pale kundi la Masahaba walipohisi kuwa wanazidiwa na matajiri katika kufanya heri hivyo wakaenda kwa Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) ili nao wapate mbinu ya kwenda sambamba na matajiri ili wasizidiwe.

Abu Swalih amesimulia kuwa, Abu Huraira (Allah amridhie) amesema: "Mafukara wa Kimuhajirina walikuja kwa Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) wakamwambia: 'Matajiri wameondokea kupata madaraja ya juu na neema za kudumu.'" Akasema (Mtume): "Kwa jambo lipi?" Masahaba wakasema: "Wanasali kama tunavyosali, wanafunga kama tunavyofunga, wanatoa sadaka nasi hatutoi (hatuna cha kutoa), wanaacha watumwa huru nasi hatuna watumwa wa kuwaacha huru."

Mtume akawaambia: "Je, niwafundishe kitu ambacho (mkikifanya) mtawakuta waliowapita na mtawapita walio nyuma yenu na hapatakuwa na yeyote ambaye ni mbora kuliko nyinyi isipokuwa yule atakayefanya kama mlivyofanya nyinyi?" Wakasema: "Tufundishe ewe mjumbe wa Allah."

(Mtume) akasema: "Mtafanya Tasbihi, Takbira na Tahmiid nyuma ya kila sala (baada ya kusali) mara 33." Abu Swalih akasema: "Muhajiruna wakarudi tena kwa Mtume wakasema, 'Ndugu zetu matajiri wamesikia tulichokifanya, nao wakafanya hivyo hivyo.'" Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) akasema: "Hizo ni fadhila za Allah humpa amtakaye." [Muslim].

Haraka ya Mtume katika mambo ya heri

Katika maisha yake yote, Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) alikuwa akiharakia kufanya mambo ya heri. Kutoka kwa Uqba bin Harith (Allah amridhie) amesema: "Nilisali sala ya Alasiri nyuma ya Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) katika mji wa Madina, (Mtume) akatoa salamu kisha akasimama haraka na kupenyua shingo za watu mpaka akafika kwenye chumba cha mkewe, watu wakafadhaishwa na haraka yake.

(Baadae) Mtume aliwatokea tena akaona kuwa wamestaajabishwa na haraka yake, akawaambia: "Nimekumbuka kipande cha dhahabu kilichokua kwetu (katika riwaya nyingine 'kipande cha sadaka') nikachukia kisije kunizuia (hivyo) nikaamrisha kigawanywe." [Bukhari]. Mtume alihofia kifo kisije kumkuta akiwa na mali ambayo alitakiwa awe ameshaitoa sadaka.

Abubakar alivyowatangulia watu katika heri

Sahaba Abubakar (Allah amridhie), ambaye pia ni Khalifa wa kwanza Muongofu wa Uislamu, alikuwa mwepesi mno kupita njia zenye heri na ujira mkubwa. Siku moja Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) aliwauliza Masahaba juu ya matendo yao ya siku.

Mtume aliwauliza: "Ni nani miongoni mwenu ameamka na funga (swaumu) leo hii?" Abubakar akasema: "Ni mimi." Mtume akauliza tena: "Ni nani leo hii amesindikiza jeneza?" Abubakar akasema: "Ni mimi." Akauliza: "Ni nani miongoni mwenu leo amemlisha masikini."

Abubakar akasema: "Ni mimi." Akauliza tena: "Ni nani miongoni mwenu leo amemtembelea mgonjwa?" Abubakar akasema: "Ni mimi." Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) akasema: "Mambo haya hayakusanyiki kwa mtu mmoja isipokuwa ataingia Peponi." [Muslim].

رمضان فتاوى

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Je, lazima kunuizwa ili kufunga Ramadhan?

Swali: **Sheikh wetu anayetunuiza amesafiri, tunampigia simu hapatikani na Mwezi wa Ramadhan ndio umeshaingia. Je, tunaruhusiwa kufunga bila kunuia au tumsubiri mpaka arudi?**

Jibu: Kwa hakika, funga ya mwezi wa Ramadhan ni ibada, na ibada yoyote ile haisihi na haikubaliki isipokuwa kwa kuwepo nia.

Allah anasema: "Nao hawakuamrishwa isipokuwa wamwabudu Allah kwa kumtakasia Dini kwa ajili Yake, wakiwa wanyoofu". Na Mtume wa Allah, (Allah amshushie rehema na amani), anasema: Kwa hakika matendo yanategemea nia."

Kwa kuwa swaumu au kujizuia na kula na kunywa kunaweza kuwa kwa mazoea, kwa kutokuwa na hamu ya chakula, kwa maradhi, kwa mazoezi, au sababu nyinginezo, basi hakutambuliki kuwa ni ibada ya swaumu ya kisheria isipokuwa kwa nia.

Amesema Imam An-Nawawi (Allah amrehemu): "Haisihi swaumu isipokuwa kwa nia. Na nia mahali pake ni moyoni, na haitakiwi kuitamka kwa ulimi bila ya ikhtilafu (wanazuoni hawakutofautiana katika hilo). Na ni wajibu kuweka nia kwa kila siku (ya swaumu). "

Katika Uislamu, nia ni kitendo cha moyoni kati yako na Mwenyezi Mungu. Si jambo linalohitaji mtu mwingine akutilishe au akusomee.

Hii inaonesha kuwa nia mahali pake ni moyoni mwa mwenye kufunga, haihitaji kutamkwa kwa sauti, haihitaji kufanywa na Sheikh wala haihitaji kushikwa mkono au kusomewa dua maalum.

Ikiwa unajua kuwa kesho ni Ramadhan na umeamua moyoni kuwa utafunga kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu, basi hiyo tayari ni nia sahihi. Nia ni yako binafsi, Inafanywa moyoni kabla ya Alfajiri na haihitaji Sheikh wala kiongozi yeyote wa kukunuiza. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Swali: **Ni yapi yanayobatilisha na kuharibu swaumu?**

Jibu: Yanayobatilisha swaumu ni mambo, mosi, kujamiiana (kufanya tendo la ndoa); pili, kula; tatu, kunywa; nne, kutokwa na manii kwa matamanio; tano, kitu chochote kilicho na maana ya kula na kunywa; sita, kutapika kwa makusudi; kutokwa na damu kwa hijama (kujikata kwa ajili ya kutoa damu) na kutoka kwa damu ya hedhi na nifasi.

Ama kuhusu kula, kunywa na kujamiiana, dalili yake ni kauli ya Mwenyezi Mungu: "Basi sasa waingilieni wake zenu na tafuteni alichokuandikieni Mwenyezi Mungu. Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe kutokana na uzi mweusi wa alfajiri. Kisha timizeni saumu mpaka usiku." [Quran, 2: 187].

Ama kutokwa na manii kwa matamanio, dalili yake ni Hadith Qudsi Mwenyezi Mungu aliposema: "Anaacha chakula chake, kinywaji chake na matamanio yake kwa ajili Yangu." Na Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Katika tendo la ndoa la mmoja wenu kuna sadaka." Swahaba wakauliza: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je mmoja wetu akitimiza matamanio yake anapata thawabu?" Akasema: "Mnaonaje kama angelifanya katika haramu, je asingepata dhambi? Basi vivyo hivyo akilifanya katika halali hupata thawabu."

Kinachowekwa (katika tendo la ndoa) ni manii yanayotoka kwa msukumo. Kwa hiyo kauli yenye nguvu ni kwamba madhii (majimaji yatokayo kabla ya manii) hayabatilishi swaumu, hata kama yametoka kwa matamanio au kwa kugusana bila kujamiiana.

Kuhusu, kilicho na maana ya kula na kunywa ni sindano za lishe (dripu) ambazo humtosheleza mtu badala ya chakula na kinywaji. Ingawa si kula wala kunywa moja kwa moja, lakini zinachukua nafasi ya chakula na kinywaji. Ama sindano ambazo hazitoi lishe wala hazichukui nafasi ya chakula na kinywaji, hizo hazibatilishi swaumu, iwe zimewekwa kwenye mshipa, kwenye misuli au sehemu nyingine ya mwili.

Ushahidi kuhusu kutapika kwa makusudi, yaani mtu ajilazimishe atoe kilichomo tumboni hadi kitoke mdomoni. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Atakayejitapisha kwa makusudi basi atalipa (ataqadha), na atakayeshindwa na matapishi (yakamtoka bila kukusudia) hana deni."

Hekima yake ni kwamba akitapika kwa makusudi tumbo hubaki tupu na mwili huhitaji chakula kufidia. Kwa hiyo ikiwa swaumu ni ya faradhi, hairuhusiwi kujitapisha kwa sababu ataharibu swaumu yake ya wajibu.

Kwenye suala la kutokwa na damu kwa hijama, ushahidi ni kauli ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Amefutari mwenye kufanya hijama na anayefanyiwa hijama." Ama kuhusu kutoka damu ya hedhi na nifasi, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Je, kwani huoni kwamba mwanamke anapopata hedhi haswali wala hafungi?" Pia, wanazuoni wamekubaliana kwenye hilo.

Mambo haya yanayobatilisha swaumu hayabatilishi ila kwa masharti matatu: Awe na elimu (ajue hukumu), awe anakumbuka (si kwa kusahau) na awe amekusudia (si kwa kulazimishwa au kwa bahati mbaya). Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

TUJIFUNZE AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

Kila mtu anaweza kufadika na AI, sio wa maofisini pekee

Kuna watu wengi leo wanaipenda AI kupita kiasi, na wapo wanaoichukia kabisa.

Binafsi yapo nisiyoyapenda kuliko AI, lakini ukweli utabaki pale pale kuwa mifumo hii ina faida nyingine, hasa katika kuturahisishia kazi.

Katika maeneo machache ambayo AI inatumika vibaya ni pale watu wanapoitumia kuandika kila kitu kwa niaba yao, hadi sauti yao halisi inapotea.

Wengine wanaitumia kuiga kazi za wasanii au kutafuta ushauri wa kitabibu bila wataalamu. Katika hali hizi ndipo matatizo yanapoanzia.

Lakini ukweli ni huu: AI si adui. Tatizo si teknolojia, bali namna tunavyoitumia.

AI haipaswi kuchukua nafasi ya juhudi zako, kipaji chako au maamuzi yako binafsi. Badala yake, inaweza kuwa zana ya kukurahisishia maisha, kukusaidia kupanga vizuri, na kukuongezea ufanisi.

Moja ya fikra potofu katika matumizi ya AI ni kuwa hii ni kwa ajili ya watu wa maofisini wanaofanya kazi za taaluma rasmi. Lakini ukweli ni kwamba kila mtu anaweza kufaidika.

Kwa Mtanzania wa kawaida – bodaboda, mama ntilie, muuza duka, mwanafunzi au mfanyabiashara mdogo – AI inaweza kuwa msaada mkubwa kama itatumika kwa makusudi sahihi.

AI, msaidizi wako wa kila siku anayekupunguzia msongo

Ingawa maisha ya wengi wetu ni ya haraka na yenye majukumu mengi, ukweli ni kwamba wengi wetu huchoka si kwa sababu ya kazi nyingi pekee, bali kwa sababu hawajajipanga vizuri.

AI inaweza kusaidia kupanga vipaumbele. Badala ya kufanya kila kitu kwa wakati mmoja, inaweza kukushauri lipi lifanywe kwanza na lipi lisubiri. Una kazi, familia, mipango na changamoto za kila siku. Badala ya kuhangaika kichwani kupanga kila kitu, unaweza kutumia AI kama msaidizi wako wa kidijitali.

AI inaweza kukusaidia kugawanya muda wako, kupendekeza mapumziko, na hata kubaini sababu zinazokufanya uchoke bila kujua. Ni kama kuwa na mshauri anayekusaidia kuona makosa madogo katika utaratibu wako.

Unaweza kuiambia AI: "Ninafanya biashara asubuhi hadi jioni, nina familia na nataka pia kujifunza ujuzi mpya. Nipangie ratiba itakayoniwezesha kufanya yote bila kuchoka kupita kiasi."

Kuongeza ufanisi katika biashara

AI inaweza kusaidia kuandika matangazo mazuri ya biashara yako. Kama wewe ni mama ntilie, unaweza kuomba ikusaidie kuandika ujumbe mfupi wa kuvutia wateja wa WhatsApp. Au kama unaona inakupoka ubunifu wako, andika mwenyewe na iombe ikuhariri.

Kama wewe ni bodaboda, unaweza kupata mawazo ya jinsi ya kujitangaza kwa lugha rahisi lakini yenye mvuto. Kwa ujumla, hakuna atakayetoka kapa bila manufaa akitumie vema mifumo ya AI.

Kujifunza bila aibu

Kuna mambo mengi tunataka kujifunza lakini tunaogopa kuuliza watu. AI inakupa nafasi ya kuuliza bila kujisikia aibu. Inaweza kukusaidia kwenye hesabu za biashara yako, lakini hata mama wa nyumbani anaweza kuuliza namna mapishi ya mlo fulani.

Kwa wanafunzi hasa wa vyuo, AI ni kama kuwa na mwalimu wa ziada anayepatikana saa zote. Unaweza kuuliza maana ya dhana au nadharia ambazo hukuzielewa darasani, na itakupa maelezo ya kukutosheleza na kwa lugha rahisi.

رمضان

KALAMU HURU

SEHEMU YA 3

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Upunjaji mizani: jinai inayohalalishwa kimyakimya katika jamii zetu

Tatfif katika elimu na malezi: upunjaji unaoharibu kizazi

Katika makala zilizopita, tumechunguza tatizo la tatfif (upunjaji) katika maisha ya kazi, ndoa na jamii kwa ujumla. Lakini tija athari mbaya zaidi huonekana pale upunjufu unapoingia katika elimu na malezi ambayo ni nguzo ya msingi ya mustakabali wa taifa letu. Tatfif katika elimu sio hitilafu ya mtu mmoja tu, bali ni udhaifu wa mfumo mzima unaoathiri kizazi kizima.

Upunjifu wa walimu na wataaluma

Elimu ni amana kuu ya jamii. Ni zawadi inayoweza kubadilisha maisha na kuunda jamii bora. Lakini upunjaji hutokea pale mwalimu anafika darasani bila maandalizi ya kutosha, akijua atapata mshahara bila kujali ubora wa ufundishaji.

Kwa upande mwingine, kuna walimu wanaokazia kujenga mazingira ya masomo ya ziada (tuition) badala ya kufundisha kwa bidii darasani. Baadhi ya shule nazo huona faida zaidi katika kupata ada ya ziada kuliko kuhakikisha mafanikio ya kweli ya mwanafunzi.

Kwa msingi huo, utaona wanafunzi wanarudia darasa mara kwa mara si kwa sababu walihitaji muda wa kusoma zaidi bali kwa sababu baadhi ya walimu wanaona hicho ni chanzo cha kipato cha ziada. Swali kuu ni hili: Je, mwanafunzi aliyeshindwa kuelewa somo katika dakika 45 za darasani ataweza kukisoma kitu kwa undani katika dakika chache za tuition? Jibu ni dhahiri: Hapana.

Hii inaonesha kwamba hoja ya masomo ya ziada (tuition) mara nyingi si suluhisho la elimu, bali ni chanzo kingine cha mapato kwa walimu au taasisi. Katika hali hii, mizani ya elimu inapunjwa: mshahara kamili unatolewa, lakini maarifa mwalimu anayoyatoa ni nusu au kiduchu.

Matokeo yake, tuna wahitimu wengi wenye vyeti, bila uelewa wa kina, bila ujuzi wa kutekeleza kazi yao kwa ubora.

Tatfif (upunjaji) wa wanafunzi

Tatfif si kosa la walimu tu. Wanafunzi wenyewe pia wana mchango. Mwanafunzi anayekwepa masomo, anayechukua 'notes' tu bila kuelewa, au kutafuta vyeti kwa njia fupi, hao pia wanapunja mizani ya elimu.

Aina hii ya wanafunzi wanakwenda kwenye mitihani bila kufanya juhudi ya kujifunza kwa kina; na bado wanafunzi hawa wanaamini kuwa matokeo yanaweza kupatikana bila kazi ngumu.

Tatizo hili hujirejeleza baadaye kazini, katika uongozi, na hata katika maisha ya ndoa:

Matokeo ya elimu yasiyolipiwa gharama halisi ya juhudi ni tabia ya kukwepa kazi kwa kadri ya maisha.

Tatfif (upunjaji) ya wazazi katika malezi

Elimu na malezi huungana; wazazi ni walimu wa kwanza wa watoto wao. Lakini upunjaji unapoingia katika malezi, mzazi anadai heshima bila kutoa muda na uelewa, anadai maadili bila kuwa mfano wa kuigwa, na anadai mafanikio bila kushiriki katika kuyatafuta kwa vitendo.

Watoto wanaokua bila mfano wa kufuata au mazingira ya kuthamini kazi ngumu hujenga hisia ya haki ya kupokea zaidi kuliko kutoa.

Upunjaji ndani ya sera

Upunjaji wa mizani hauko tu kwa walimu au wanafunzi; pia umejificha ndani ya sera na taratibu za taasisi.

Mfano ni mitaala isiyozingatia uhalisia: Sio kila kitabu au somo vinahusiana na maisha halisi ya mwanafunzi. Kuna shule zinazoangazia zaidi ukusanyaji wa ada kuliko ubora wa elimu ambapo ada zinapewa kipaumbele kuliko mafanikio ya mwanafunzi. Huo ni mfumo unaopunja mizani.

Kuna tathmini zinazoipa uzito dhana ya kukariri kuliko kufikiri, ambapo kunapimwa kumbukumbu badala ya uelewa wa kina. Hii ni hatari kwa ubora wa elimu, jambo ambalo linapelekea jamii kulipa gharama ya elimu lakini elimu hiyo wanayoipata haiwaandai kwa maisha halisi.

Athari za tatfif (upunjaji) katika elimu

Matokeo ya upunjaji wa mizani katika elimu ni mengi, makubwa na ya kina ikiwemo uwepo wa vyeti vingi bila ujuzi wa kutekeleza kazi; utaalamu dhaifu unaoathiri ubora wa huduma na uzalishaji; uzembe unaorithiwa kizazi hadi kizazi, na jamii iliyojengwa juu ya misingi dhaifu ya maendeleo.

Kwa ufupi, jamii inayokubali upunjaji wa mizani katika elimu huwa inajenga msingi dhaifu wa maendeleo yake yenyewe.

Namna ya kuondosha upunjaji

Mambo kadhaa yanaweza kufanyika ili kurejesha mizani katika elimu na kuondoa upunjaji. Katika hayo ni pamoja na kurejesha elimu kama amana thabiti, si biashara ya vyeti tu na kuwekeza katika uadilifu kabla ya matokeo.

Mengine yanayoweza kufanyika ni walimu, wanafunzi na wazazi kufahamu wajibu wao kwa pamoja, tathmini katika ufundishaji iwe ya kuibua ufahamu na ujuzi wa kutatua matatizo, si kukariri tu; na mitaala iweze kuendana na uhalisia wa maisha na soko la ajira.

Kwa hiyo trunachosema ni kuwa elimu yenye mizani imetokana na maarifa, maadili, na uwajibikaji.

Hitimisho na Muendelezo

Tatfif katika elimu ni upunjaji wa kimya unaoandaa taifa kwa migogoro ya kijamii, kiuchumi na kimaadili. Pale elimu inapopunjwa, hakuna sekta inayoweza kusimama imara.

Katika makala inayofuata, tutaangazia Tatfif katika biashara na uchumi kuanzia sokoni, mikataba, zabuni hadi mifumo ya kifedha, na jinsi tabia hii inavyoathiri uaminifu wa kiuchumi katika jamii.

Usikose makala inayofuata.

رمضان

MAKALA MAALUM

0712 690 811

NA SHEIKH SEIF RUGA

Nyudhuru za kisheria zinazoruhusu kuacha kufunga Ramadhan

Sharia ya Allah, Mwingi wa Hekima na Mjuzi wa kila kitu imekuja ikiwa kamili kwa mahitaji ya mwanadamu; inarekebisha maisha yake, inanyoosha upotovu wa nafsi yake, na wakati huo huo huzingatia udhaifu wake na ubinadamu wake pamoja na hali mbalimbali zinazompata na kumuathiri. Ndiyo maana Uislamu umejengwa juu ya msingi wa wepesi, huruma na upole katika sharia zake zote.

Sharia ya Uislamu haiwalazimishi wafuasi wake yale wasiyoyaweza. Allah Mtukufu anasema: "Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim..." [Qur'an, 22:78]. Kadhalika Allah anasema: "Mwenyezi Mungu anataka kukupeni yaliyo mepesi wala hataki kukupeni yaliyo mazito." [Qur'an, 2:185].

Swaumu ni ibada inayohitaji subira na ustahimilivu. Wapo watu katika jamii yetu ambao hawamudu kufunga katika hali fulani. Kwa mujibu wa kanuni ya Uislamu ya kurahisisha na kuondoa uzito, Allah Mtukufu amewaruhusu baadhi ya waja wake kuacha kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa kuwahurumia na kuwapunguzia uzito.

Msafiri

Msafiri ameruhusiwa kutofunga mchana wa Ramadhan ikiwa safari hiyo ni ya halali na haina maasi ndani yake. Allah Mtukufu anasema: "Basi atakayekuwa miongoni mwenu mgonjwa au yuko safarini atimize idadi katika siku nyingine..." [Qur'an, 2:185].

Huu ni ushahidi wa wazi kwamba msafiri anaruhusiwa kufungua swaumu na atalazimika kulipa siku alizoacha kufunga baada ya Ramadhan. Sheria ya Kiislamu imehusisha kupunguza sala na kuruhusu kufungua swaumu katika safari kwa ujumla, bila kutaja umbali maalumu.

Hata hivyo, kwa kuwa mara nyingi safari huambatana na mashaka ambayo kwa kawaida hupatikana katika safari ndefu, wanazuoni wamekhitalifiana katika kubainisha umbali unaoruhusu msafiri kuacha kufunga.

Wapo waliosema kuwa umbali unaoruhusu kufungua swaumu ni wa safari ya siku mbili kamili au zaidi kwa mwendo wa ngamia au miguu, unaokadiriwa kuwa takriban kilomita 80. Na kuna waliosema kuwa hakuna umbali maalumu; kila inayoitwa safari katika desturi za watu ('urf) ni halali kufungua swaumu.

Kauli yenye nguvu katika suala hili ni ya kwanza, kwa kuwa safari ya siku mbili huhitaji maandalizi na pia ndani yake kuna mashaka yaliyo wazi. Lililo bora kwa msafiri ni kufanya lililo jepesi kwake kati ya kufunga na kufungua.

Ikiwa vyote viwili ni sawa kwake (hakuna ugumu wowote), basi kufunga safarini ni bora zaidi ili kupata fadhila ya wakati wa Ramadhan. Hata hivyo, ikiwa kufunga kunamsumbua au kumletea mashaka, basi inampasa asifunge safarini.

Ikiwa mtu amekusudia kukaa zaidi ya siku nne katika mji fulani kwa ajili ya masomo, biashara, au mambo mengine ya halali, basi atawajibika kufunga swaumu na kusali sala kamili kama wakazi wengine, kwa kuwa hukumu za safari zinakuwa zimekatika kwake.

Na kama amekusudia kukaa siku nne au chini ya hapo, au amekaa kwa ajili ya haja fulani bila kujua lini ataondoka, basi anaruhusiwa kufungua swaumu, kwa kuwa hukumu za safari bado hazijakatika kwake.



MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 2

SIMULIZI YA AKINA THAMOUD WATU WA NABII SWALEH

VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

Tulijifunza katika toleo lililopita namna kina Thamoud walivyolewa na starehe na walivyozama katika maasi, yakiongozwa na kibri na ushirikina wa kuabudu masanamu waliyoyatengeneza wenyewe. Ndio hapo Allah akamtoa miongoni mwao mjumbe aliyeitwa Swaleh, awatoe gizani na kuwapeleka kwenye nuru.

Vipaumbele vya da'wa ya Mtume Swaleh (amani ya Allah imshukie) ilikuwa ni vile vile vya Mitume wengine, navyo ni Tawhid, vikiongozwa na Imani juu ya uwepo Allah, Muumba wa kila kitu mneemeshaji, anayestahiki kuabudiwa na kushukuriwa.

Kipaumbele kingine ni imani juu ya maisha ya akhera, yaani watu kufufuliwa, kuhesabiwa na kulipwa kwa mujibu wa matendo yao. Huko akhera, wema kuingizwa katika bustani takatifu, humo watakuta kila linaloburudisha nyoyo, macho na viwiliwili vyao. Waovu kuingizwa katika maisha ya milele motoni, humo watakutana na kila aina ya adhabu ya kuwaumiza. Tunamuomba Allah atuhifadhi waja wake.

Upinzani wa Thamoud

Kama walivyofanya kina Adi kwa Mtume wao Hud, wakuu (waheshimiwa) wa kina Thamoud walikaidi mafundisho ya Mtume wao, wakamkejeli, kumdhihaki na kumcheka.

Walihoji iweje mtu masikini asiye na majumba na mashamba anakuwa mtume? "Wakasema, 'Oh! Tumfuate mtu mmoja miongoni mwetu! Kwa hakika tutakuwa katika upotofu vichaa. Oh! Ameteremshiwa yeye tu ukumbusho baina yetu, bali yeye muongo na mwenye kujiona." Allah akasema: "Watakuja kujua kesho yupi muongo ajionae'" [Qur'an, 54:24-27].

Alipozidi kuwaonya na adhabu ya Allah, watu wake walimwambia: "Wewe Saleh, ulikuwa kijana mwema. Tulikuwa tunakutegemea utakuwa miongoni mwa watu muhimu katika jamii yako! Umetuvunja moyo na kutupotezea matumaini yetu kwako!" Qur'an inasema: "Wakasema, 'Ewe Swaleh, kwa hakika ulikuwa wa kutarajiwa (sana) kwetu kabla ya haya (sasa umeharibika). Unatukataza kuabudu waliowaabudu baba zetu? Na hakika sisi tuko (katika nyoyo) na shaka kwa haya unayotuitia." [Qur'an,11:62].

Na alipowapitia wakiwa kwenye barza zao, walioneshana kwa vidole vyao na kutoa maneno ya kejeli wakisema: "Mungu amsaidie baba Swaleh, maskini! mwanawe ameharika (amepotea)."

Mtume Swaleh aliyasikia maneno yao, akaona namna watu wake walivyozama katika kuipenda dunia na starehe zake, na akawasikitikia sana.

Wakuu kuwazuia wanyonge kumuamini Swaleh

Wakuu na matajiri wa jamii ya Mtume Swaleh walipowaona watu wameanza kumsikiliza waliwakataza. Qur'an inasema: "Na wakubwa katika watu wake waliokufuru na kukadhibisha makutano ya akhera na ambao tuliwatajirisha katika maisha ya dunia walisema, 'Hakuwa huyu ila mtu kama nyinyi, anakula katika vile mnavyokula, na anakunywa katika vile mnavyokunywa. Na kama mkimtii mtu kama nyinyi, mtakuwa wenye kupata khasara. Anakuahidini ya kwamba mtakapokufa na mkawa udongo na mifupa kuwa mtatolewa (mtafufuliwa)? Hayawi hayawi haya mnayoahidiwa, hakuna (mengine) ila maisha haya ya dunia, tunakufa na kuishi, wala sisi si wenye kufufuliwa'" [Qur'an, 23:33-37].

Mazingatio

Huu unaitwa "ushetwani" ufanywao na wakuu wa jamii pale wanapojitokeza wanaolingania watu katika dini ya Allah. Ni husda itokayo ndani ya nyoyo zao, pale wanapowaona wengine wana hamu ya kuijua na kuifuata njia (dini) ya haki.

Kuwazuia watu kuijua na kuifuata haki ni jarima (kosa) kubwa mbele ya Allah. Kwani hilo ni jambo la khiari ya moyo.

Mtu anapokataa ukweli kisha akawazuia wengine wasiukubali, anafananishwa na joka la mdimu kwenye mto. Watu huogopa hata kusogelea, wala joka nalo halina shida ya ndimu wala kuteka maji! Hii ni dhambi kubwa kwa kweli.

Mwenyezi Mungu anawaelezea watu kama hawa: "Hakika waliokufuru hutoa mali zao ili kuzuia (watu kuamini) njia ya Allah, basi watazitoa kisha majuto yatakuwa juu yao, kisha watashindwa, na wale waliodumu juu ya ukafiri watakusanywa katika Jahannam." [Qur'an, 8:36].

Na katika sura nyengine, Allah anasema: "Wakasema wakuu wa kaumu yake waliotakabari kuwaambia wale walio dhaifu, wenye kuamini miongoni mwao, 'Je mnaitakidi ya kwamba Swaleh ametumwa (amepewa utume) na Mola wake?' Wakasema, 'Hakika sisi tunaamini yote aliyotumwa kuyafikisha.' Wakasema waliotakabari, 'Sisi tunayakataa yote mnayoyaamini.'" [Qur'an, 7:75-76].

رمضان

NASAHA ZA WIKI

0787 503 085

NA YUSUFU AMINI

Zingatia haya kuboresha funga yako

Ndugu yangu Muislamu, Ramadhan ni msimu bora wenye kheri nyingi kuliko misimu yote katika mwaka. Hivyo basi, ni wajibu wetu kutumia fursa hii kubwa aliyotuneemesha Mola wetu katika kumtii na kujikurubisha kwake kwa kila aina ya wema, tukimuiga Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani imshukie).

Kila mtu anahitaji kufanya mambo mema na mazuri kwa nia ya kujipendekeza (kujikurubisha) kwa Mwenyezi Mungu na kujiongezea thawabu na malipo, kwani thawabu za Allah hazina mipaka. Kwa kuzingatia hayo, yafaa kila Muislamu ajibidiishe katika kutenda amali nyingi za kheri ndani ya mwezi huu wa Ramadhan.

Na ili swaumu iwe na maana na yenye kufikia lengo, mfungaji hana budi kuepuka makosa yafuatayo ambayo hupunguza thawabu kwa wafungaji wengi ndani ya mwezi wa Ramadhan.

Maneno machafu

Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) amesema: "Yule ambaye anamuamini Allah na Siku ya Mwisho, aseme jambo la kheri. Kama hana, ni vema akanyamaza." [Bukhari na Muslim]. Hali kadhalika, Mtume alisema kumwambia Muadh (Allah amridhie): "Tahadhari na kiungo hiki," Mtume akiashiria ulimi wake. [Tirmidhi].

Hatari ya ulimi inaongezeka zaidi katika mwezi wa Ramadhan wakati mtu akiwa amefunga. Makosa yanayosababishwa na ulimi ambayo huiathiri swaumu ya mtu ni mengi, ikiwamo kusema uongo, kusingizia, kusengenya, kufitini, kutukana, kubishana na kadhalika.

Sharia tukufu ya Kiislamu imetoa muongozo kwa waja wake waliofunga, ikiwa ni njia ya kuitakasa nafsi ya mfungaji na kuikinga na swaumu yake na uovu huo: "Na iwapo mtu atamtusi basi na aseme, 'Hakika mimi nimefunga.'" [Bukhari na Muslim].

Kuacha kusali jamaa

Wanazuoni wa Elimu ya Kiislamu wameafikiana kwa pamoja ya kuwa sala ya jamaa ni miongoni mwa mambo yaliyosisitizwa mno katika dini. "Na shikeni sala na toeni zaka, na inameni pamoja na wanaoinama." [Qur'an, 2:43].

Sasa ni vipi swaumu inaweza kunyooka kwa mtu asiyesali pamoja na Waislamu wenzake, au hasali kabisa!? Tunajilinda kwa Allah na hali hiyo. Kama mtu hasali, swaumu yake inakosa mizania kwa Allah Aliyetukuka!

Kufanya israfu ya chakula

Furaha huwafanya watu wengi waipokee Ramadhan kwa kufanya ufujaji wa vyakula na vinywaji hadi inafikia hatua kudhani huu ni msimu wa kuoneshana ubingwa katika fani ya mapishi.

Allah anakataza fujo katika matumizi: "Na kunyweni na wala msifanye ubadhirifu. Kwa hakika Yeye (Allah) hawapendi wafanyao israfu." [Qur'an, 7:31]. Ni wajibu kwa kila mfungaji kuweka ulinganifu katika upande huu na kuacha kufanya israfu na ufujaji katika vyakula na vinywaji.

Kuacha kula daku

Kuacha kula daku ni kosa jingine ambalo watu wamezoea kulifanya. Mtu asiyekula daku anakosa fursa ya kupata baraka na malipo makubwa yanayopatikana kwa kula daku katika wakati wake muafaka.

Anas (Allah amridhie) kasimulia kutoka kwa Zaid bin Thabit ambaye amesema: "Tulikula daku na Mtume (rehema za Allah na amani imshukie), kisha tukaswali." Nikauliza: "Kuna urefu gani baina ya muda wa daku na adhana?" Mtume akajibu: "Urefu wake ni ule wa kutosha kusoma aya hamsini za Qur'an." [Bukhari na Muslim]. Hivyo, kila Muislamu anapaswa kufuata nyayo za Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) kwa kula daku.

Kutouthamini mwezi huu Mtukufu

Kuna baadhi ya watu hawauthamini na kuupa hadhi mwezi wa Ramadhan. Hili ni jambo la hatari na la kushangaza, kwa sababu Waumini wa kweli ni wale ambao wanauthamini mwezi wa Ramadhan na kuupa hadhi yake inayostahili. Vilevile, Waumini wa kweli hawapuuzii fadhila za Ramadhan na umuhimu wake.

Kwa hao wapuuzaji tunaowajua, Ramadhan haina jipya isipokuwa kujizuia kula na kunywa tu. Aghlabu wapuuzaji hawa hutumia wakati wao mwingi katika yale yanayotia raha katika nafsi zao na husalia katika hali yao hiyo hadi Ramadhan inamalizika na kujikuta katika majuto na hasara.

Hawa, watapata majuto na hasara kwa sababu kuidiriki Ramadhan nyingine ni majaliwa ya Allah. Mtume ametwambia: "Amekula hasara mtu ambaye ameidiriki Ramadhan na ikaondoka, kisha asisamehewe madhambi yake." [Tirmidhi].

Kulala kupita kiasi

Hiki ni kitendo kibaya kinachofanywa na wafungaji wengi katika mwezi wa Ramadhan. Muda mwingi wa mchana huutumia kulala fofofo na hufanya hivyo kwa sababu walikesha usiku kuangalia filamu, tamthilia, mpira, au katika baraza za kahawa. Pia wengine hulala mchana ili kupunguza makali ya njaa na kiu.

Madhara ya ulalaji wa aina hii ni kushindwa kusali katika wakati wake. Watu hawa wauchapao usingizi mchana ili kupata fursa ya kukesha katika majilisi za kahawa na pumbao wamekula hasara isiyomithilika. Allah Aliyetukuka anasema: "Enyi mliyoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na kila nafsi iangalie inayoyatanguliza kwa ajili ya Kesho." [Qur'an, 59:18].

Kuacha kusali Tarawehe

Baadhi ya watu hawataki kusali Tarawehe, sala ya Sunna ambayo Waislamu huitumia kujisogeza kwa Mola wao kutafuta msamaha wa madhambi kwa kuomba na kunyenyekea. Kuna watu wanaoacha kusali Sunna ya Tarawehe kwa madai kuwa siyo sala ya wajibu. Huko ni kujikosesha thawabu na fadhila zinazopatikana ndani ya Ramadhan.

Kuufanya msimu wa pumbao

Ewe Muislamu, Ramadhan ni msimu wa ibada, kuchota fadhila, utiifu, kujikuribisha kwa Allah; na kamwe siyo msimu wa michezo ya pumbao, kama wafanyavyo baadhi ya watu ambao hawachezi karata au dhumna isipokuwa ndani ya Ramadhan tu.

Hayo ni mambo ya haramu na yenye kuwapotezea fadhila na ujira upatikanao katika mwezi huu. Watu hao wangeweza kuutumia mchana wao kuvuna thawabu kwa kusoma Qur'an, kusoma vitabu vya dini, kusikiliza mawaidha na kadhalika. Na ifikapo jioni wangeutumia muda wao kusali Tarawehe, na pia kupumzika ili waweze kuwahi sala ya Alfajiri.

رمضان

MAKALA MAALUM

0783 650 803

SAID RAJAB

Falsafa ya funga ya Ramadhan

Ramadhan ni mwezi wa tisa katika Kalenda Tukufu ya Kiislamu (Al–Hijri), na ndiyo mwezi pekee uliotajwa kwa jina lake ndani ya Qur'an. Kiuhalisia, kufunga mwezi wa Ramadhan ni nguzo ya nne kati ya nguzo tano za Uislamu.

Kabla ya Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie) na Masahaba wake (Allah awaridhie) hawajaamrishwa kuondoka Makka na kuweka makazi Madina, Waislamu walikuwa wakifunga zile funga ambazo hazikuwa za faradhi.

Ulipofika mwaka wa pili Hijriya (623 A.D) ndipo mfululizo wa aya katika sura ya pili ya Qur'an Tukufu (kuanzia aya ya 183 mpaka 187) zikawaamrisha Waislamu kufunga mwezi wote wa Ramadhan na kanuni za msingi za ibada hii zikawekwa.

"Enyi mliyoamini! Mmeandikiwa swaumu, kama walivyoandikiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu. (Mfunge) siku maalumu za kuhesabika. Na atakayekuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku nyingine. Na wale wasioweza (kufunga) watoe fidia kwa kumlisha masikini. Na atakayefanya wema kwa kujitolea, basi ni bora kwake. Na mkifunga ni bora kwenu ikiwa mnajua.

"Mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uongofu na upambanuzi. Basi atakayekuwa mjini katika mwezi huu na afunge. Na ambaye ni mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku nyengine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hesabu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongoeni ili mpate kushukuru.

"Na waja wangu watakapokuuliza habari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya muombaji anaponiomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi ili wapate kuongoka." [Qur'an, 2:184–186].

Baada ya sala, wajibu wa pili ambao kila Muislamu anatakiwa kuutekeleza ni kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Neno 'swaum' ambalo limetumiwa ndani ya Qur'an na hadith kwa kufunga, maana yake ni kujizuia. Kwa hiyo, farasi ambaye anajizuia kutembea tembea, au kula chakula chake anatajwa kuwa 'swa'im'.

Katika lugha ya kitaalamu au tuseme kisharia, swaumu inaashiria kufunga au kujinyima chakula, vinywaji na kujamiiana, kuanzia mapambazuko ya jua hadi machweo yake. Kufunga, kama taasisi ya utakaso wa roho, ni jambo la kawaida kwa dini zote hata zile zinazodai kuwa ni za kiungu (Divine Religions).

Mwandishi wa makala kuhusu 'kufunga', katika Encyclopadia Britannica anaeleza kwamba: "Itakuwa vigumu sana kutaja mfumo wowote wa kidini, kwa maelezo yoyote yale ambayo 'kufunga' hakutambuliki kabisa." Taasisi hii ilikuwa imara miongoni mwa Mayahudi na Wakristo.

Kumbukumbu za hadith zinatoa ushahidi wa kutosha kuhusu ukweli kwamba kufunga ilikuwa ni desturi ya kidini iliyozoeleka miongoni mwa Waarabu wa kabla ya Mtume Muhammad. Na walikuwa wakifunga tarehe 10 ya mwezi wa Muharram, kwa sababu ilikuwa ni siku ambayo Mwenyezi Mungu alimuokoa Nabii Musa na watu wake kutoka kwenye makucha ya Firauni, ambaye alizamishwa baharini pamoja na jeshi lake.

Waarabu na watu wengine, pia walikuwa wakifunga swaumu kama tendo la toba, au upatanisho, au ibada ya matayarisho kabla ya tendo fulani la kula, au tambiko, au sherehe ya maombolezo.

Katika Uislamu, kufunga, kimsingi ni taasisi ya nidhamu ya kiroho na kujitawala (self control). Kwa hakika ni zoezi la kujitoa kidini kwa namna ya kukataa kwa hiari, ndani ya muda fulani, tamaa zote za mwili zilizo halali. Zile tamaa za haramu, bila shaka zimeshakataliwa moja kwa moja. Qur'an inasema: "Enyi mliyoamini! Mmeandikiwa swaumu, kama walivyoandikiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu." [Qur'an, 2:183].

Siwezi kukushinda kwa jambo lolote milele

Zaid bin Aslam amepokea hadith kutoka kwa baba yake kuwa, siku moja alimsikia Umar bin Khattwab (Allah amridhie) akisema: "Mtume wa Allah (rehema.na amani zimshukie) alituamuru tutoe sadaka katika wakati ambao nilikuwa na mali, nikasema, 'Leo nitahakikisha namshinda Abubakar kama itatokea (itawezekana) kumshinda, nikaja na nusu ya mali yangu.'" Mtume (rehema na amani zimshukie) akaniuliza: "Umebakiza nini kwa ajili ya familia yako?" Nikajibu: "Nimebakiza mfano wa hiyo niliyotoa (nusu iliyobaki)." Kisha Abubakar akaja na mali yake yote, Mtume (rehema na amani zimshukie) akamuuliza: "Umebakiza nini kwa ajili yao?" Akasema: "(Familia yangu) nimewaachia Allah na Mtume wake (yaani hakubakiza kitu)." Umar akasema: "Sitaweza kukushinda kwa jambo lolote milele."

Mafundisho ya tukio hili:

Tukio hili linaonesha pupa waliyokuwa nayo wema waliotangulia katika suala la kujitolea mali zao katika milango ya kheri. Ilikuwa kawaida kujitolea sehemu ya mali yao kwa ajili ya Allah Mtukufu na kutekeleza lengo la uwepo wao duniani.

Aghlabu Mtume (rehema na amani zimshukie) alipowahamasisha Masahaba kujitolea kwa ajili ya kuipambania dini ya Allah, hawakusita hata kidogo kuitikia wito huo. Kila mmoja alidhamiria kumshinda mwenzake na kumtangulia katika kheri hiyo.

Hivi sasa tuko ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan, mwezi wa kujipinda na kujitoa kwa dhati katika kila aina ya kheri iliyopo mbele yetu. Pamoja na wingi wa mambo ya kheri ambayo ni fursa kwa kila Muislamu kujibidiisha kuyafanya, kuna mambo ambayo msingi wake ni kujitolea mali katika njia ya Allah kwa ajili ya kujikurubisha kwake ndani ya siku bora za mwezi huu wa Ramadhan.

Kutoa sadaka

Kutoa sadaka ni ibada bora inayomkurubisha mja kwa Allah Ta'ala hasa ndani ya mwezi wa Ramadhan. Katika nukuu mbalimbali za Sunna, tunajifunza namna Mtume (rehema na amani zimahukie) alivyokuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia watu. Masahaba (Allah awaridhie), nao hawakubaki nyuma katika kuiga mwenendo huu wa Mtume.

Tunaelezwa kuwa, mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie) alikuwa mkarimu kuliko watu wote, na alikuwa mkarimu zaidi katika mwezi wa Ramadhan. Ukarimu wake katika kufanya mambo ya kheri ulikuwa kama upepo unaovuma kwa kasi. Mtume amesema: "Sadaka iliyo bora zaidi ni ile inayotolewa katika (mwezi wa) Ramadhan." [Tirmidhi kutoka kwa Anas].

Hadith nyingine kutoka kwa Talha bin Yahya inaeleza kwamba, bibi yake aitwae Su'da bint Awf (mke wa Talha bin Ubaydillah) alisema: "Siku moja Talha aliingia kwangu akiwa na huzuni, nikamuuliza: 'Mbona naona uso wako umebadilika? Je, kuna jambo nimekufanyia?'"

Akasema: "Hapana, wewe ni mke mwema." Nikamuuliza: "Kuna nini basi?" Akasema: "Mali niliyonayo imekuwa nyingi na imeniletea mzigo moyoni." Nikamwambia: "Basi igawanye." Akaigawa mali hiyo kiasi ambacho haikubaki hata dirhamu moja, ingawa kabla ya hapo alikuwa na dirhamu 400,000.

Naam! Hivi ndivyo Mtume na Masahaba wake walivyotuachia alama na athari njema ya namna Muislamu anavyotakiwa ajitolee mali yake katika njia ya Allah. Sadaka katika mwezi wa Ramadhan ina fadhila ya kipekee.

Unaweza kutoa sadaka ndani ya mwezi wa Ramadhan kadri ya uwezo wako kwa sura nyingi, ikiwamo kulisha watu chakula. Allah Mtukufu anasema: "Na wanawalisha chakula pamoja na kukipenda, masikini, yatima na mateka. (Wanasema): Hakika sisi tunakulisheni kwa ajili ya Allah tu, hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunamuogopa Mola wetu kwa siku yenye shida na taabu. Basi Allah akawalinda na shari ya siku hiyo, akawakutanisha na nuru na furaha, na akawalipa kwa uvumilivu wao Pepo na hariri." [Qur'an, 76:8–12].

Wema waliopita walikuwa wanahimiza sana kulisha watu chakula, na waliitanguliza huduma hii juu ya ibada nyingi. Haishurutishwi umlishe fukara tu, hata kumlisha ndugu mwema ni kheri pia. Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Enyi watu! Toeni salamu, lisheni chakula, dumisheni undugu, na swalini usiku watu wakiwa wamelala, mtaingia Peponi kwa amani." [Ahmad na Tirmidhi].

Miongoni mwa watu waliopendelea sana kulisha watu chakula ni Abdullah bin Umar (Allah amridhie). Sahaba huyu Mtukufu alikuwa anafungua swaumu (anakula futari) pamoja na mayatima na masikini. Kadhalika, Masahaba wengine wengi walikuwa wanawalisha na kuwahudumia wenzao. Kulisha watu chakula hupandikiza mapenzi baina ya ndugu na ni sababu ya kuingia Peponi. Pia hutoa fursa ya kukaa na watu wema na kupitia chakula hicho hupata nguvu ya kufanya ibada.

Jambo hili linaunga na kutia nguvu undugu, ujirani na ujamaa, kwani kupitia mwaliko wa chakula wanakutana masikini na matajiri, marafiki, na hata wale wasiojuana hutokea kufahamiana katika matukio ya namna hii. Kulisha chakula ni takrima inayopendwa na watu wengi kutokana umuhimu wake katika kujenga upendo na ujamaa, ambao ni vigumu kuujenga kwa njia nyingine. Ikiwa mtu hawezi kulifanya hilo kwa kiwango cha kuwakusanya watu wengi, basi afanye hivyo hata kwa mtu mmoja au wawili, kwani Allah humlipa mtu kwa nia yake na uthubutu wake wa kufanya hivyo kwa ajili ya kutaka radhi zake.

Kufuturisha waliofunga

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Atakayemfuturisha aliyefunga anapata malipo (thawabu) mfano wa malipo ya aliyemfuturisha, na hakipungui chochote katika malipo ya mfungaji." [Ahmad na Nasai].

Kuna njia nyingi za kuwafuturisha watu; unaweza kuandaa chakula cha futari na kuwakaribisha watu waje kula, au kuandaa kitu chochote ambacho unahisi kuwa ni bora kwa mfungaji na ni rahisi kukitumia kwa ajili ya kufungua kinywa, mfano tende, maji au matunda mengine ambayo ni mwafaka.

Si lazima kuandaa chakula kingi na kuwaalika watu ili kupata fadhila za kufuturisha, hapana! Fadhila hizi utazipata kwa kujipanga vizuri kwa kuhakikisha kuwa unaandaa chochote ambacho ni rahisi kutumika kwa ajili ya kufungua kinywa.

JUNAYNAT ALLY DAMA

Ramadhan, fursa ya kuimarisha mahusinao ya kifamilia

Nyumba ni kimbilio la amani. Ndani yake ndipo wazazi na watoto wanapaswa kujenga mapenzi, heshima na mawasiliano ya wazi.

Hata hivyo, kasi ya maisha ya sasa na matumizi makubwa ya mitandao ya kijamii vimechangia kupungua kwa mazungumzo ya ana kwa ana ndani ya familia nyingi. Kila mmoja anakuwa na ratiba na simu yake, na hivyo mshikamano wa familia kudhoofika taratibu.

Kwa mujibu wa mafunzo katika tovuti noja ya Kiislamu ya nchini Misri, Dar Al-Ifta, mwezi wa Ramadhan ni fursa adhimu ya kurejesha mawasiliano, kuimarisha mapenzi na kujenga upya roho ya familia.

Ramadhan si mwezi wa kufunga tu, bali ni mfumo wa maisha unaofundisha nidhamu, ushirikiano na huruma.

Moja ya njia kuu ya kuimarisha mshikamano wa familia ni kuishi Ramadhan kwa malengo ya pamoja.

Funga inalenga kumjengea muumini taqwa—kumcha Mwenyezi Mungu katika kila jambo. Wazazi na watoto wanapokubaliana kushirikiana katika ibada, kuswali pamoja na kusaidiana katika mema, nyumba hubadilika na kuwa sehemu ya kujifunza maadili. Hali hii huondoa migongano isiyo ya lazima na kuleta mazungumzo yenye kujenga.

Mjumuiko wa Iftar ni nyenzo nyingine muhimu ya kuimarisha mapenzi ya kifamilia. Jioni familia hukusanyika mezani kuvunja swaumu kwa tende na maji, wakifuata mwenendo wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake).

Kitendo hiki huleta furaha ya pamoja na hisia ya kukamilisha wajibu wa siku. Mazungumzo ya mezani, kushirikiana chakula na kuombeana dua huongeza mawadah (mapenzi ya dhati). Ndiyo maana inapendekezwa Ramadhan iwe mwezi wa kula zaidi nyumbani kuliko nje, ili kuipa familia kipaumbele.

Njia nyingine ni kuanzisha mkusanyiko wa kila siku kwa ajili ya kuisoma Qur'an. Familia inapoketi pamoja kusoma au kusikiliza aya chache kila siku, hujenga utulivu wa ndani na maadili ya pamoja. Mkusanyiko huu unaweza kuambatana na kusoma tafsiri nyepesi ili watoto waelewe maana ya aya na kuzitumia katika maisha yao. Huu ni uwekezaji wa kiroho unaoimarisha uhusiano wa wazazi na watoto.

Vilevile, kwenda msikitini pamoja kwa Swala ya Tarawehe hujenga kumbukumbu za kiimani na kuzoesha watoto ibada ya jamaa. Safari hizi za pamoja huimarisha ukaribu wa kihisia kati ya mzazi na mtoto, na kuifanya Ramadhan kuwa uzoefu wa familia nzima, si wa mtu mmoja mmoja.

Ushirikiano katika maandalizi ya Iftar na daku ni njia nyingine ya kukuza upendo na uwajibikaji. Wazazi wanapowapa watoto majukumu madogo jikoni au katika kuandaa meza, wanawajengea hisia ya kuthamini familia yao.

Ushirikiano huu hupunguza lawama na kuongeza heshima kwa juhudi za kila mmoja.

Ramadhan pia ni wakati wa kufundisha huruma na sadaka. Kuwahimiza watoto kutoa kwa wahitaji au kuwashirikisha katika kugawa chakula hujenga moyo wa kujali wengine. Familia inaposhirikiana katika matendo ya kheri, mshikamano wao huongezeka kwa sababu wanahisi wanatekeleza lengo moja. Aidha, kuimarisha undugu na ujirani ni sehemu ya kuijenga familia. Ziara fupi kwa ndugu kwa ajili ya kumpelekea jirani chakula huongeza upendo na kuondoa tofauti ndogo ndogo. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alihimiza kupeana zawadi kwa kuwa huongeza mapenzi.

Katika siku za mwisho za Ramadhan, familia inaweza kushirikiana katika maandalizi ya Sikukuu ya Eid—kusafisha nyumba, kupamba na kununua mavazi ya watoto. Shughuli hizi huleta furaha na kujenga kumbukumbu zitakazodumu kwa miaka mingi.

UKHTI FATIMA SS

Faida za kisaikolojia za funga ya Ramadhan

Kila mwaka, mamilioni ya Waislamu duniani hufunga mwezi wa Ramadhan kama sehemu ya ibada yao. Mbali na umuhimu wake wa kiroho, mwezi huu pia unaleta faida nyingi za kisaikolojia ambazo huathiri fikra, hisia na tabia ya mtu kwa njia chanya.

Kwa kuzingatia makala zilizotolewa na tovuti za Chama cha Madaktari wa Kisyria Wanaoishi Nje ya Nchi (The Syrian Expatriates Medical Association – SEMA) na pia Autralian Muslim Times (AMUST), tunaweza kuona wazi jinsi funga ya Ramadhan inavyoweza kuimarisha afya ya akili na ustawi wa mtu.

Kwanza kabisa, funga ya Ramadhan hufundisha utawala wa nafsi na kujidhibiti. Mtu anapojifunza kusubiri bila kula au kunywa kwa saa nyingi kila siku, anajifunza pia kudhibiti hisia kama hasira, tamaa au hali ya kukosa subira.

Kwa hiyo funga si suala la kukaa na njaa tu bali ni zoezi la kujifunza kukaa kimya na kutokutoa majibu haraka kwa hali zote za maisha. Kwa kufanya hivi kila siku, mtu hujenga uwezo wa kukabiliana na msongo wa mawazo, hali ya kuchanganyikiwa na msukumo wa haraka wa hisia.

Mbali na kujidhibiti, Ramadhan pia inachochea afya bora ya hisia. Kwani mfungo huleta mabadiliko ya maisha, ikimsukuma mtu kuwa mtulivu zaidi, kufanya tafakari za ndani zaidi, na kuenzi wakati wa kuishi kwa undani. Kwa mfano, ibada kama kusoma Qur'an, kusali kwa utulivu, na kumbukumbu za Allah husaidia kuondoa mawazo yanayochanganya na kumuacha mtu akiwa na hali ya kutulia zaidi.

Afya bora ya hisia inasaidia kupunguza shinikizo la mawazo, mfadhaiko au hisia za kuchanganyikiwa ambazo wengi katika hali ya kawaida hujaribu kupambana nazo kupitia vilevi au shughuli za burudani zisizo na tija.

Kwa upande mwingine, Ramadhan huongeza huruma kwa wengine. Kufikiria juu ya njaa na kiu ya watu masikini au walio katika hali ngumu kunamaanisha kuwa mtu anapata ukaribu wa kihisia na wengine. Hii huongeza uwezo wa huruma, kuwakumbuka wenye hali ngumu — tabia ambayo inachangia mtiririko mzuri wa hisia na ustawi wa ndani. Taifa lolote lenye moyo wa huruma hutengwa na jamii yenye hisia za upendo na mshikamano.

Aidha, funga ya Ramadhan huwezesha mtu kupata shukrani na mtazamo mzuri wa maisha. Kwa kujizuia na vitu vingi vya dunia, mtu anapata nafasi ya kutambua kwamba ana mengi ya kushukuru — kama afya, familia, marafiki na mali nyingine za kijamii.

Tabia hii ya kutambua baraka za pamoja inaweza kupunguza hisia za kutoridhika, kukosoa maisha au kulinganisha ustawi kuelekea hali hasi. Kwa kufanya hivi kila siku, mtu anaweza kubadilisha mtazamo wake wa maisha kwenda kwa njia ambayo inachangia ustawi wa akili yake.

Faida nyingine muhimu ni uwezo wa kusawazisha hisia na tabia. Ramadhan inamhimiza mtu kutafakari juu ya matendo yake, maneno anayosema na jinsi anavyowasiliana na wengine. Hii inawawezesha watu kupunguza tabia za kuharibu mahusiano kama kutumia maneno ya kuudhi au kuonesha dharau kwa wengine.

Tabia hizi mbaya mara nyingi huongeza msongo wa mawazo na kuvuruga amani ya ndani, lakini kupitia mchakato wa kufunga na kutafakari, mtu anaweza kuzibadilisha kwa tabia chanya. Pia, Ramadhan humpa mfungaji maana na lengo la maisha-kutafuta radhi za Allah Aliyetukuka. Watu wengi wanapokosa mwelekeo au wanapopitia huzuni, Ramadhan inaweza kuwa mwamba wa kuibua tena roho na kujenga upya imani.

Kujihusisha katika ibada, kutoa sadaka, kushiriki katika jamii na kufanya kazi za huruma kunatengeneza mtazamo wa maisha ambao unaweka kipaumbele cha kufanya mema kuliko kutafuta mafanikio ya dunia tu. Hii inaweza kuchangia kupunguza hisia za upweke, kutokua na maana au kujihisi mtu hana thamani.

Katika mwezi huu pia hali ya upweke huoungua kwa sababu kuna matukio mengo yatakuleta karibu na watu – aidha familia au marafiki na jamaa. Kwenyee familia, kuna kufuturu pamoja, kwenda msikitini pamoja, kupika kwa pamoja na bado hujazungumzia mialiko ya futari.

NA UKHTI FATIMA

Biashara zinazoweza kukuingiza pesa nzuri Ramadhan hii

Kwanza kabisa, ni muhimu kusisitiza jambo moja: kuingia kwa Ramadhan hakumaanishi kwamba kazi husimama. Kufunga hakutuhitaji kuacha majukumu, tena sanasana yanazidi.

Kumbuka, watu bado wana familia za kuhudumia, ada na nauli za watoto kwenda shule, kodi za nyumba na mahitaji ya kila siku. Hivyo, kutafuta riziki ni wajibu unaoendelea hata ndani ya mwezi mtukufu.

Kwa wenzangu na mimi wa sekta isiyo rasmi, ukweli ni kwamba "Bongo inabidi ichemke" zaidi katika Ramadhan . Sababu ni rahisi—mahitaji huongezeka. Kuanzia kwenye chakula cha Iftar na daku, tende, juisi, nafaka, hadi mavazi ya Sikukuu ya Eid, soko linapanuka. Huu si mwezi wa kulala; ni mwezi wa kujipanga, kuongeza ubunifu na kufanya kazi kwa maadili. Kufanya haya pia ni ibada kubwa.

Ramadhan hubadilisha mwenendo wa matumizi ya watu. Familia hununua zaidi vyakula vya jioni, taasisi na misikiti huandaa Iftar za pamoja, na watu wengi hujiandaa kwa Sikukuu mapema. Hivyo, mfanyabiashara makini anaona fursa badala ya changamoto.

Kwa wale wanaofikiria kutumia upekee wa mwezi huu kujitafutia kipato—iwe kwa kuboresha biashara iliyopo au kuanzisha mpya—zifuatazo ni fursa zinazoweza kuzingatiwa:

Pesa ilipo mwezi huu

Biashara ya vyakula vya ni mojawapo ya fursa kubwa. Sambusa, maandazi, uji, juisi za asili, matunda na tende vinahitajika kila jioni. Ukiwa na mtaji mdogo unaweza kuanza nyumbani na kuuza mtaani au kupokea oda kwa simu.

Huduma ya kutoa huduma ya futari kwa oda kubwa kwenye shughuli maalum (catering) ni fursa nyingine yenye faida. Makampuni, vikundi na familia huandaa Iftar za pamoja. Ikiwa una ujuzi wa kupika na mtandao mzuri wa wateja, unaweza kupata oda nyingi kwa mwezi mzima.

Biashara ya tende ni maalum kwa Ramadhan . Tende ni chakula kinachopendekezwa wakati wa kufuturu, hivyo mahitaji yake hupanda sana. Unaweza kuuza kwa jumla au kwa vifurushi maalumu vya zawadi.

Uuzaji wa juisi na vinywaji vya asili ni biashara yenye mzunguko wa haraka. Baada ya siku ndefu ya kufunga, watu huhitaji kinywaji cha kurejesha nguvu. Juisi za ukwaju, embe, nanasi au tikiti maji zina soko kubwa.

Biashara ya mavazi ya Kiislamu kama kanzu, hijabu, baibui na nguo za watoto hupata wateja wengi kabla ya Eid. Ukiwa na mtaji mdogo unaweza kuwa wakala bila kuhifadhi mzigo mkubwa.

Huduma za ushonaji pia huongezeka mahitaji yake. Wateja wengi hupendelea kushona nguo za Eid kwa mtindo wao binafsi.

Biashara ya vifurushi vya Ramadhan na Eid pia ni wazo zuri. Unaweza kuandaa vikapu vyenye tende, keki, kahawa, vifaa vya ibada au bidhaa za nyumbani kwa ajili ya zawadi. Mtu ananunua kikapo kizima na kumpelekea yoyote amtakaye kama zawadi.

Vifaa vya ibada kama misahafu, mikeka ya kuswalia, tasbihi na kofia hupata soko kubwa katika mwezi huu.

Mapambo ya nyumbani kama taa za fanusi, vyombo vya mezani na mapazia pia huhitajika kwa familia zinazopamba nyumba kwa ajili ya Iftar na Eid.

Mwisho, unaweza kuboresha biashara yako ya kawaida kwa kuongeza bidhaa maalumu za Ramadhan kama vifurushi vya nafaka au "Ramadhan combo packs" kwa bei ya kuvutia.

Mbinu chache za kuzingatia

Kwanza, chagua biashara inayoendana na mtaji na uwezo wako. Usifuate mkumbo bila kufanya tathmini ya soko lako na mazingira unayofanyia kazi.

Tambua walengwa wako ni nani. Je, unalenga wanafunzi, wafanyakazi, familia au taasisi? Uelewa huu utakusaidia kupanga bei na matangazo sahihi.

Chagua muda sahihi wa kuuza. Biashara ya futari ifanyike karibu na muda wa kufuturu. Chakula cha daku kiuzwe usiku sana alfajiri kwa hiyo uwe tayari kuchelewa kulala. Ratiba sahihi huongeza mauzo.

Tumia promosheni na punguzo maalumu za Ramadhan . Watu wengi huvutiwa na ofa za "nunua mbili pata moja" au punguzo la bei kwa oda kubwa.

Fikiria kuuza mtandaoni na ana kwa ana. Tumia WhatsApp, Instagram au Facebook kutangaza bidhaa zako huku ukiendelea kuhudumia wateja dukani au mtaani.

Hakikisha huduma ni ya haraka na ya kirafiki. Tabasamu, heshima na usafi vinaweza kumfanya mteja arudi tena au akutangaze kwa wengine.

Jenga uaminifu. Usipandishe bei kiholela kwa sababu ya mahitaji kuongezeka. Ramadhan ni mwezi wa maadili, na sifa njema itakusaidia hata baada ya mwezi kuisha.

Kwa kifupi, Ramadhan ni mchanganyiko wa ibada na juhudi halali za kutafuta riziki. Kazi haisimami. Mahitaji yanaongezeka. Ukiwa na mpango, ubunifu na maadili mema, mwezi huu unaweza kuwa wa baraka si tu kiroho bali pia kiuchumi.